SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI OFISIYA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA MWAL. HAROUN ALI SULEIMAN (MBM)

KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MEI, 2018

YALIYOMO

UTANGULIZI 1

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018..... 4

G01- Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora 6

Taasisi Zinazopokea Ruzuku 16

G02 – Mahakama 21

G03 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu 25

G04 – Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka..... 27

G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria..... 28

G06 – Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali 29

G07 – Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi 30

G08 – Kamisheni ya Utumishi wa Umma 32

G09 – Tume ya Utumishi Serikalini 33

MUELEKEO WA PROGRAMU ZA OFISI YA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 34

Vipaumbele vya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 34

Malengo Makuu ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2018/2019 36

G01 – Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora 37
Taasisi Zinazopokea Ruzuku 43
G02 – Mahakama 45
G03 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali 46
G04 – Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka 47
G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria 47
G06 – Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali 48
G07 – Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi 49
G08 – Kamisheni ya Utumishi wa Umma 49
G09 – Tume ya Utumishi Serikalini 50

SHUKURANI 51
HITIMISHO 54
Kiambatanisho 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha, 2017/18 (katika ,000) 55
Kiambatanisho 2: Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2018/19 (,000) 58
Kiambatanisho 3: Makusanyo ya Mapato kwa Julai/Machi 2017/2018 na Makadirio ya 2018/2019 61
Kiambatanisho 4: Upatikanaji wa Fedha za Maendeleo kwa Kipindi cha Julai 2017 - Machi 2018 62
Kiambatanisho 5: Miradi ya Maendeleo 2018/2019 63

Kiambatanisho 6a:- Ufunguaji wa Kesi Mahakamani
2017/2018 64
Kiambatanisho 6b: Ufunguaji wa Kesi katika Mahakama
za Mwanzo 2017/2018 68
Kiambatanisho 6c: Ufunguaji wa Kesi katika Mahakama
za Kadhi 2017/18 70
Kiambatanisho 7a: Malalamiko ya Watumishi Kuanzia
Julai – Machi 2017/2018 71
Kiambatanisho 7b: Watumishi Walioajiriwa Kuanzia
July, 2017 Hadi Kufikia Machi, 2018 72
Kiambatanisho 7c: Shughuli Za Tume ya Utumishi
Serikalini 2017/2018 74
Kiambatanisho 8a: Idadi ya Wafanyakazi ORKSUUUB
Machi 2018 78
Kiambatanisho 8b: Idadi ya Wafanyakazi katika Taasisi
Zinazojitegemea 2018 79

HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MWAL. HAROUN ALI SULEIMAN (MBM) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako Tukufu sasa likae kama Kamati kwa madhumuni ya kupokea, kujadili na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

2. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kukutana hapa leo katika Baraza hili Tukufu tukiwa salama katika hali ya amani na utulivu.

3. **Mheshimiwa Spika,** baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, naomba nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuliongoza vyema Taifa letu na kutuletea maendeleo katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiutamaduni. Uongozi wake imara na makini umeiwezesha Serikali kutekeleza kwa kiwango kikubwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 hadi 2020. Hakika mwelekeo huu ndio nguzo ya kufikia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar inayoelekeza nchi yetu kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2020. Vilevile, kwa namna ya kipekee

naomba kumpa pongezi za dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, kwa kutimiza azma yake aliyoahidi wakati wa kuinadi Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya kuongeza maslahi ya watumishi wa umma kutoka kima cha chini cha Shilingi laki moja na hamsini hadi kufikia kima cha chini cha Shilingi laki tatu.

4. **Mheshimiwa Spika,** nachukua nafasi hii pia kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi kwa kuendelea kumshauri vyema Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, nikupongeze wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, na Wenyeviti wa Baraza, kwa kuliongoza vyema na kwa umahiri mkubwa Baraza letu la Wawakilishi. Vilevile, ninawapongeza Wenyeviti na Wajumbe wa Kamati mbali mbali za Baraza, kwa kufanya kazi zao kwa uadilifu, umakini na weledi. Kamati hizi zimeweza kutoa ushauri na maelekezo yanayosaidia sana utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zetu kwa manufaa ya wananchi wetu.

5. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Hassan Hafidh Khamis, Mwakilishi wa Jimbo la Welezo kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Mheshimiwa Dkt. Makame Ali Ussi, Mwakilishi wa Jimbo la Mtopepo kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Kuteuliwa kwao na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kuwasaidia Mawaziri husika kuongoza Wizara hizo ni dalili tosha juu ya uwezo walionao, katika kusaidia utekelezaji wa majukumu ya wizara hizo kwa lengo la kuwaletea maendeleo endelevu wananchi wa Zanzibar.

6. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii maalum kuishukuru Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalumu ya Baraza la Wawakilishi chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Machano Othman Said, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Mfenesini na Makamo wake Mheshimiwa Mwantatu Mbaraka Khamis, Mwakilishi wa Viti Maalumu wa Mkoa wa Kusini Unguja kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano mzuri iliyotupatia wakati wa kupitia Muhtasari wa Taarifa ya utelekezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 na Mapendekezo ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

7. **Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mheshimiwa Miraji Khamis Musa, Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) Mwakilishi wa Jimbo la Chumbuni, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Shaibu Said Ali Mwakilishi wa Jimbo la Chonga, pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa ushauri, maelekezo na ushirikiano mzuri waliotupa wakati wa kupitia Muhtasari wa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 na Mapendekezo ya Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

8. **Mheshimiwa Spika,** napenda kumshukuru Naibu Waziri Mheshimiwa Khamis Juma Mwalim, Mwakilishi wa wananchi Jimbo la Pangawe kwa kunisaidia vyema kutekeleza majukumu ya Ofisi hii.

9. **Mheshimiwa Spika,** nitakuwa sijatenda haki iwapo sitomshukuru kwa dhati kabisa Dkt. Abdulhamid Yahya

Mzee, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi ambaye pia ni Kiongozi wa Utumishi wa Umma Zanzibar kwa maelekezo na ushirikiano mzuri ulioiwezesha Wizara hii kutekeleza majukumu yake ya kuwatumikia watumishi wa umma na wananchi kwa jumla.

10. **Mheshimiwa Spika,** kwa dhati na kwa upendo mkubwa niwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Makunduchi kwa kuendelea kuniunga mkono na naomba waendelee kunipa ushirikiano. Kwa upande wangu na mimi nitaendelea kushirikiana nao kuhakikisha kuwa maendeleo yanapatikana. Aidha, ninaishukuru familia yangu kwa msaada wanaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku. Bila ya ustahamilivu na ushirikiano wao nisingeweza kuitendea haki nafasi hii.

11. **Mheshimiwa Spika,** baada ya shukrani hizo, naomba sasa niwasilishe utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na mwelekeo wa malengo ya mwaka wa fedha 2018/2019.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

12. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2017/2018, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliidhinishiwa jumla ya Shilingi 21,563,210,200.00 kwa kazi za kawaida ambapo makadirio ya mishahara yalikuwa Shilingi 13,480,810,200.00 na matumizi mengineyo yalikuwa Shilingi 8,082,400,000.00. Hadi kufikia mwezi Machi 2018, kiasi cha Shilingi 15,773,157,034.00 kilipatikana kwa matumizi ya kawaida,

zikiwemo Shilingi 10,211,308,735.00 za mishahara sawa na asilimia 76 na Shilingi 5,561,848,299.00 za matumizi mengineyo, sawa na asilimia 69.

13. **Mheshimiwa Spika**, shughuli za maendeleo zilitengewa Shilingi 2,025,382,000.00 ambapo Shilingi 1,000,000,000.00 ni mchango wa Serikali na Shilingi 1,025,382,000.00 kutoka Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP). Kiasi cha fedha za maendeleo kilichopatikana ni Shilingi 180,000,000.00 kutoka Serikalini na Shilingi 94,080,000.00 zilipatikana kupitia mchango wa UNDP katika utekelezaji wa Mradi wa Mabadiliko katika Sekta ya Sheria.

14. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ruzuku Ofisi ilikadiriwa kutumia Shilingi 2,245,900,000.00 na hadi kufikia Machi 2018, Ofisi imepokea Shilingi 1,677,111,683.00 sawa na asilimia 75. Kwa upande mwingine, Ofisi ilikadiria kukusanya Shilingi 714,639,000.00 ili kuchangia mapato ya Serikali. Hadi Machi 2018, fedha zilizokusanywa ni Shilingi 446,322,439.00 sawa na asilimia 62 ***(angalia viambatanisho nam. 1,3&4).***

15. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inasimamia Mafungu tisa ambayo ni G01-Ofisi Kuu; G02 Mahakama; G03-Ofisi ya Mwanasheria Mkuu; G04-Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka; G05-Tume ya Kurekebisha Sheria; G06-Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; G07-Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi; G08-Kamisheni ya Utumishi wa Umma na G09-Tume ya Utumishi Serikalini. Maelezo yafuatayo yanahusu utekelezaji wa malengo katika mafungu haya tisa ya Ofisi

ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

G01- Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

16. **Mheshimiwa Spika,** Fungu la G01 linahusu Programu tano ambazo ni Programu ya Usimamizi wa Watumishi wa Umma; Programu ya Uimarishaji Mawasiliano ya Serikali; Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora; Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Aidha, katika fungu hili la G01 kuna Programu ndogo tisa na hadi kufikia Machi 2018 Programu hizo zilitekeleza yafuatayo: -

Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma

17. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma inatekeleza programu ndogo mbili ambazo ni Maendeleo ya Rasilimali Watu na Maendeleo ya Miundo na Mifumo ya Taasisi. Programu ndogo ya Maendeleo ya Rasilimali Watu ina lengo la kuendeleza mipango ya upatikanaji wa watumishi wenye sifa watakaopelekea kutoa huduma bora kwa wananchi.

18. **Mheshimiwa Spika,** mafunzo kwa watumiaji wa mfumo wa kieletroniki wa taarifa za watumishi, mafunzo juu ya muongozo wa uandaaji viongozi katika utumishi wa umma na mafunzo ya muongozo wa tathmini ya mafunzo Unguja na Pemba yametolewa. Aidha, vikao vya majadiliano ya mpango wa miaka mitano wa rasilimali watu kwa Wizara na Taasisi za Umma na tathmini ya utekelezaji wake kwa

mwaka 2017/2018 vimefanyika na hatimaye kuidhinisha mpango wa mwaka 2018/2019.

19. **Mheshimiwa Spika,** vikao vya Wakurugenzi Uendeshaji na Utumishi vimeratibiwa na kusimamiwa ili kujadili masuala ya kiutumishi. Aidha, watendaji wanne wameshiriki Mkutano wa Jumuiya ya Kiafrika ya Uongozi na Utawala wa Umma na kupata fursa ya kujifunza na kupata uzoefu wa mbinu za uendeshaji wa shughuli za kiutumishi. Mwongozo wa tathmini ya mafunzo umetayarishwa na mafunzo juu ya muongozo huo yametolewa kwa Wakurugenzi wa Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakurugenzi wa Mabaraza ya Miji na Halmashauri na Maafisa Utumishi wa Wizara na Taasisi zote za Umma.

20. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuliarifu Baraza lako Tukufu kwamba, kupitia Programu hii ndogo, Ofisi inakamilisha maandalizi ya kuwahamisha rasmi watumishi 9,611 kwenda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka katika Sekta za Elimu (7,922), Afya (1,201) na Kilimo (488), ili kuanzia mwezi Julai 2018, watumishi hao wawe chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Hatua hii inafanywa kufuatia tathmini ya ugatuzi iliyofanywa na Kamati tano zilizoundwa na Serikali.

21. **Mheshimiwa Spika,** programu ndogo ya Miundo na Mifumo ya Taasisi ina lengo la kuimarisha mfumo wa miundo ya kiutumishi na maslahi ya watumishi. Kazi ya kuwapanga watumishi wa umma katika miundo ya utumishi kwa mujibu wa sifa za kielimu, vyeo na uzoefu wa

kazi alionao mtumishi imefanyika. Vilevile yamefanyika marekebisho ya mishahara kwa kada ya maofisa utumishi, marekebisho ya pencheni za wastaafu wa kawaida pamoja na mazingatio ya pencheni kwa watumishi waliokuwa katika nafasi za uteuzi wa Mheshimiwa Rais. Programu hii pia imetayarisha na kupendekeza malipo ya posho za safari za nje katika utumishi wa umma na imesimamia kupata ufumbuzi wa malipo ya viinua mgongo kwa watumishi wa Idara Maalumu za SMZ. Jambo jengine la msingi lililotekelezwa ni kuwasilisha serikalini ripoti ya malipo ya mshahara na posho kwa watumishi wa Mashirika, Mamlaka na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

22. **Mheshimiwa Spika,** uelewa kuhusu upimaji wa utendaji kazi kwenye Wizara na Taasisi za Serikali umetolewa, mapitio na kazi ya kuandaa miundo ya utumishi kwa Wizara na Taasisi za Serikali yamefanyika pamoja na kuwajengea uwezo maofisa wa Idara ya Miundo ya Taasisi.

23. **Mheshimiwa Spika,** shughuli nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na kutayarisha na kutoa ufafanuzi kuhusu miongozo, matoleo yanayohusu utumishi wa umma, utekelezaji wa Sera ya Malipo ya Watumishi wa Umma na Wanasiasa, kufuatilia utekelezaji wa Mkataba wa Utoaji wa Huduma kwa Mteja katika Wizara na Taasisi za Serikali, pamoja na kushiriki katika kazi ya Tathmini ya Kazi na Madaraja kwa mujibu wa uzito wa kazi husika *(Job Evaluation and Grading Exercise)*.

Programu ya Uimarishaji wa Mawasiliano ya Serikali

24. **Mheshimiwa Spika**, umuhimu wa kuunganisha mfumo wa malipo ya mishahara na ule wa usimamizi wa rasilimali watu umeelezwa vyema kwenye Mkakati wa Mabadiliko ya Utumishi wa Umma Zanzibar. Katika kipindi hiki, hatua zilizochukuliwa ni maandalizi ya mfumo wa malipo ya mishahara utakaounganishwa na mfumo wa usimamizi wa rasilimali watu *(an integrated human resource and payroll system)*. Katika kipindi hiki hatua zilizokwisha tekelezwa ni pamoja na kuandaa mfumo wa malipo ya mishahara ambao unaipa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora uwezo wa kusimamia mfumo huo moja kwa moja. Hivi sasa upo katika majaribio kwenye ORKSUUUB, Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Mfumo huo utakapokamilika utaziwezesha Wizara na Taasisi za Serikali kupata taarifa za watumishi wao kwa wakati na kuziwezesha taasisi kusimamia idadi halisi ya watumishi. Hali hii itasaidia usimamizi mzuri zaidi wa kiwango cha mahitaji na malipo ya mishahara (wage bill). Katika kuimarisha mfumo wa kitaasisi, Idara imeandaa rasimu ya sheria ya uanzishwaji wa Wakala wa Serikali Mtandao ambayo inatarajiwa kupelekwa katika kikao cha Makatibu Wakuu.

Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora

25. **Mheshimiwa Spika,** programu ya Usimamizi wa Utawala Bora ina lengo la kuimarisha misingi ya utawala bora katika utekelezaji wa Taasisi za Serikali. Mikutano na semina za kuelimisha Masheha, vituo vya elimu, na wananchi kwa jumla imefanyika. Jarida la kwanza la Utawala Bora limechapishwa na kusambazwa kwa wahusika mbali mbali.

Jumla ya vipindi 28 vimeandaliwa na kurushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji ZBC na vipindi sita kupitia Redio Jamii Mkoani Pemba. Aidha, elimu imetolewa kwa kamati 52 za ushauri za Masheha na taasisi mbili za elimu kisiwani Pemba.

26. **Mheshimiwa Spika**, makongamano ya utawala bora yaliyofanyika Unguja na Pemba yameleta hamasa kwa wahusika kuzingatia utawala bora katika shughuli zao. Vilevile, Serikali za Mitaa zilijengewa uwezo kuifahamu misingi ya utawala bora kwa kuwashirikisha Watendaji na Waheshimiwa Madiwani wa Mamlaka zote za Serikali za Mitaa Unguja na Pemba. Aidha, walimu wanaosomesha somo la uraia wamejengewa uwezo kupitia mikutano minne iliyofanyika katika vituo vya walimu. Sera na Mpango Mkakati wa Utawala Bora zinafanyiwa mapitio na rasimu ya awali inatarajiwa kukamilika katika mwaka 2017/2018.

27. **Mheshimiwa Spika,** suala la ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar limekuwa likisisitizwa na viongozi wetu. Idara, katika mwaka huu wa fedha, ilifanya ziara maalum katika Manispaa ya Dodoma kwa lengo la kupata uzoefu juu ya namna manispaa hiyo inavyotekeleza majukumu yake kwa kuzingatia misingi ya utawala bora.

Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini

28. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini ina lengo la kuratibu na kusimamia shughuli zinazoihusu Ofisi ya Mufti kwa kutoa Fatwa na kutoa miongozo kuhusu masuala ya dini. Migogoro ya kidini

imetatuliwa, kuratibu na kusimamia vikao vya Baraza la Ulamaa, Kamati ya Kitaifa ya kuthibitisha kuandama kwa mwezi, na kujibu maswali ya Dini ya Kiislam ya wananchi. Ziara za misikiti na vyuo vya Qur-ani zilifanyika kwa lengo la kuratibu shughuli za taasisi hizo.

29. **Mheshimiwa Spika,** katika kuendeleza jitihada za kuwa na takwimu sahihi za idadi na hali ya madrasa na misikiti hapa Zanzibar, Ofisi ya Mufti imesajili madrasa 104 na Misikiti 61 Unguja na Pemba. Ukaguzi umefanyika katika vyuo vya Qur-ani 58 na misikiti 50 na mashauriano kuhusu changamoto yamefanyika ambapo ushauri ulitolewa kuhusu maendeleo ya taasisi hizo. Pamoja na hayo, Ofisi imepokea mgogoro mmoja wa madrasa na migogoro tisa ya misikiti. Kati ya migogoro hiyo, minne imetatuliwa na migogoro mitano inaendelea na ufumbuzi. Aidha, jumla ya migogoro 63 ya ndoa, mitano ya urithi na migogoro tisa inayohusu nasabu za watoto na familia imepokelewa na kupatiwa ufumbuzi. Vilevile vikao vya Kamati ya Kitaifa ya kuthibitisha kuandama kwa Mwezi na kikao cha Baraza la Ulamaa vimefanyika.

30. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mufti imeendelea kutoa elimu na nasaha kwa wananchi. Jumla ya masuala 149 yanayohusu talaka, 47 ya ndoa, matatu ya mirathi, suala moja la hiba na moja la kupotea baharini yamejibiwa. Vipindi vya maswali na majibu vinaendelea kutolewa ambapo jumla ya maswali 74 yamejibiwa, vipindi 93 vya maswali na majibu na vipindi vya mawaidha ya Dini ya Kiislamu vimerushwa kupitia ZBC Redio. Vipindi hivyo vilihusu masuala ya ndoa, ulezi wa watoto, na uhusiano wa dini mbali mbali.

31. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha mahusiano na taasisi nyengine, Mufti na Katibu wake walihudhuria Kongamano la kidini la Afrika Mashariki na Kati lililoandaliwa na Jumuiya ya 'Islamic Foundation' kwa lengo la kukuza mahusiano na viongozi wa dini wa kanda hii. Aidha, Ofisi imempokea Balozi mpya wa Saudia nchini aliyekuja Ofisi ya Mufti kujitambulisha na kubadilishana mawazo na viongozi wa Ofisi hii. Vilevile Katibu wa Mufti alihudhuria Mkutano uliotayarishwa na 'Inter Religions Council for Peace in Tanzania' kwa lengo la kuimarisha ushirikiano kwa taasisi za dini ili kuimarisha amani na utulivu.

32. **Mheshimiwa Spika,** kwa kushirikiana na 'Save the children' na 'Faith Associates' ya Uingereza Ofisi ya Mufti imekamilisha taratibu za kuandaa mtaala wa kufundishia katika madrasa za Qu-raani. Taasisi hizo tayari zimeshakabidhi nakala za vitabu vya mtaala huo kwa Ofisi ya Mufti na kinachosubiriwa ni uzinduzi wa mtaala huo ambao utasaidia kuwa na mfumo mmoja wa masomo ya ufundishaji katika madrasa zote.

33. **Mheshimiwa Spika,** vitendo vya udhalilishaji katika madrasa za Qur-ani, vimekua vikiripotiwa mara kwa mara. Kwa kipindi hiki kesi mbili za udhalilishaji zimeripotiwa na katika jitihada za kukabiliana na changamoto hizo, Ofisi ya Mufti imefanya mikutano miwili iliyojumuisha walimu wa madrasa na viongozi wa kidini. Aidha mkutano wa kuhamasisha amani na utulivu nchini umefanyika.

Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

34. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inatekeleza programu ndogo tatu ambazo ni Uongozi na Utawala, Mipango, Sera na Utafiti na Uratibu wa Masuala ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Pemba.

35. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uongozi na Utawala ina lengo la kutoa huduma za Ofisi, kusimamia Watumishi wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kuratibu shughuli za Ofisi kwa ufanisi. Vikao vitatu vya Kamati ya Uongozi, vinne vya Kamati Tendaji, viwili vya Bodi ya Zabuni, vitatu vya Kamati ya Zabuni, viwili vya Kamati ya Ukaguzi na vikao viwili vya Washirika wa Maendeleo vimefanyika. Vikao hivyo vilijadili masuala mbali mbali kuhusiana na ushirikiano na utekelezaji wa majukumu ya Taasisi na Idara za Wizara.

36. **Mheshimiwa Spika,** semina na mafunzo mbali mbali yakiwemo mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka, mafunzo ya kuandaa mpango wa rasilimali watu, mafunzo ya kuandaa mpango wa mafunzo, mafunzo ya uingizaji wa taarifa za watumishi katika mfumo wa kielektroniki na mafunzo ya mpango wa urithishaji wa uongozi yametolewa. Aidha, watumishi 11 wakiwemo wanawake wanane na wanaume watatu wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi nchini India, Zimbabwe na Uingereza na watumishi kumi wakiwemo wanawake watatu na wanaume saba wanaendelea na mafunzo ya

muda mrefu katika vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi. Programu hii imeendelea kuratibu masuala ya utumishi ambapo kwa kipindi cha hadi kufikia Machi 2018, Ofisi ina jumla ya watumishi 1,280 inayojumuisha watumishi 255 wa Idara na watumishi 1,025 wa Taasisi za Wizara ***(angalia viambatanisho nam. 8a&b).***

37. **Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Rasilimali Watu wa miaka mitano na Mpango wa Urithishwaji wa Uongozi 'Succession Plan' imeandaliwa. Aidha, nakala 400 za ziada za Mkataba wa Utoaji wa Huduma kwa Wateja wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora zimechapishwa kwa lengo la kuufahamisha umma huduma zinazotolewa na viwango vya utoaji wa huduma hizo. Mpango wa Mafunzo utakaotumika kuanzia mwaka 2018/2019 upo katika maandalizi. Kwa upande mwingine, huduma za uendeshaji zimetolewa zikiwemo upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo ya gari na jengo la Ofisi.

38. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti ina lengo la kuimarisha shughuli za Mipango, Sera na Utafiti na Usimamizi wa Programu na Miradi ya Ofisi. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na kuandaa taarifa za utekelezaji za vipindi vya robo mwaka vya 2017/2018 pamoja na kuandaa mpango wa mwaka 2018/2019. Programu ya Marekebisho ya Sekta ya Sheria imeratibiwa kwa kukamilisha mapitio ya sheria ya adhabu na sheria ya mwenendo wa makosa ya jinai ambazo zimepitishwa na Baraza la Wawakilishi. Vilevile, Sera ya Msaada wa Kisheria imepitishwa rasmi na rasimu ya Sheria ya Msaada wa Kisheria, Sera ya Nyaraka na Sera ya Mafunzo zipo katika hatua za kupelekwa Serikalini. Maofisa Mipango

wamejengewa uwezo katika kufanya uchambuzi wa sera ili kuwawezesha kutekeleza vyema kazi zao. Mafunzo mengine yaliyotolewa kwa maofisa mipango wa idara na taasisi za Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora yalihusu kuwakumbusha kuhusu maandalizi ya mpango na bajeti, ufuatiliaji na tathmini na umuhimu wa kuwa na takwimu sahihi za masuala yanayohusu Idara na taasisi za Ofisi.

39. **Mheshimiwa Spika,** shughuli za utafiti zilizotekelezwa ni pamoja na Utafiti wa Uhakiki wa Mali za Wakfu, Utafiti mdogo uliofanywa kwa lengo la kupata taarifa zitakazosaidia utaratibu wa kuanzisha *'Law School in Zanzibar'* na Tathmini ya Mwenendo wa Utekelezaji wa Programu ya Mabadiliko ya Sekta ya Sheria. Aidha, imefanyika tathmini na ukaguzi wa mifumo na vifaa vya TEHAMA kwenye taasisi 17 kwa Unguja na Pemba.

40. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Kuratibu Shughuli za Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina lengo la kutoa huduma za ofisi, kusimamia watumishi na kuratibu shughuli za Ofisi Kuu Pemba.

41. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2018, ofisi imeendelea kuwa kiungo muhimu cha shughuli za Wizara kisiwani Pemba kwa kuratibu shughuli za kitaifa, kazi za Kamati za Baraza la Wawakilishi pamoja na kufuatilia masuala ya kiutendaji kwa idara na taasisi za Wizara na hatimaye kutoa taarifa wizarani.

42. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ilikuwa ikisimamia pia utekelezaji wa Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa

na Ofisi ya Hakimiliki. Katika mwaka 2017/2018, Ofisi hizi zilishirikiana vyema na Ofisi yetu katika kutekeleza majukumu yake ambayo ni pamoja na kutoa ushauri wa utunzaji na uhifadhi bora wa kumbukumbu za serikali na kusimamia hakimiliki za wasanii na wabunifu. Kutokana na mabadiliko ya muundo wa wizara yaliyofanyika hivi karibuni, Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa imepelekwa katika Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale na Ofisi ya Hakimiliki imepelekwa katika Wizara ya Vijana, Utamaduni Sanaa na Michezo. Maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa Idara hizi yatatolewa na Wizara husika.

Taasisi Zinazopokea Ruzuku

43. **Mheshimiwa Spika,** Fungu la G01 lina taasisi tatu zinazopokea ruzuku ambazo ni: Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Chuo Cha Utawala wa Umma, na Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Utekelezaji wa majukumu katika taasisi hizo ni kama ifuatavyo: -

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana

44. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Usimamizi wa Masuala ya Dini imeendelea kuimarisha kazi za kusimamia Mali za Wakfu, Amana, Mirathi ya Waislamu, Sala na Mabaraza ya Iddi Kitaifa, Hijja, Zakka na Misaada ya kheri. Katika mwaka 2017/2018 ilijipangia kutoa huduma zilizo bora ili kuendana na mahitaji ya jamii.

45. **Mheshimiwa Spika,** katika urithishaji wa mali za marehemu waislamu, jumla ya tirka 1,073 zimefunguliwa, tirka 639 za mirathi zenye thamani ya Shilingi

16,589,178,708 zimefungwa na warathi kupewa haki zao. Aidha Kamisheni imetoa ushauri wa kisheria kwa kesi 61, imetatua mizozo 26 na 61 kupelekwa mahakamani kwa kutolewa hukumu.

46. **Mheshimiwa Spika,** tathmini ya mali, kumbukumbu na taratibu za uendeshaji wa shughuli za Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana inafanyika na iko katika hatua za mwisho. Kazi hii ikikamilika itafanya huduma hizi kutolewa kwa njia za kisasa kabisa na kuongeza tija kwa wanufaika. Jumla ya nyumba zote 307 zimekaguliwa mara mbili, nyumba 21 zimefanyiwa matengenezo yaliyogharimu Shilingi 124,466,020.00, kodi ya Shilingi 287,233,100.00 ya nyumba na Shilingi 4,930,000.00 za mapato ya mashamba imekusanywa.

47. **Mheshimiwa Spika,** zakka na misaada ya kheri yenye thamani ya Shilingi 396,885,000.00 imekusanywa na kugawiwa kwa wanufaika. Vilevile Kamisheni imeendeleza mahusiano na ushirikiano na taasisi za kidini ndani na nje ya nchi, imefanikisha upatikanaji wa misaada ya kheri na kuzisaidia taasisi za kiislamu zinazojishughulisha na utoaji misaada.

48. **Mheshimiwa Spika,** Sala na Baraza la Idd el Hajj kitaifa limeratibiwa na kwa mwaka huu lilifanyika Wilaya ya Maghribi B katika viwanja vya Mji mpya wa Fumba. Vilevile, Kamisheni imeendelea kuratibu shughuli za ofisi ya Hijja Tanzania, Kamati ya Hijja Zanzibar na Taasisi za Hijja kwa mujibu wa ratiba na miongozo iliyopo. Jumla ya mahujaji 1,077 kati ya mahujaji 1,906 wa Tanzania nzima walisafirishwa na taasisi za Zanzibar. Maandalizi kwa ajili ya ibada ya Hijja ya mwaka 1438AH sawa na 2018 yanaendelea vyema. Aidha, waraka wa kuundwa Mfuko

wa Hijja umeshawasilishwa Wizarani kwa kuanza taratibu za kisheria.

49. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya vipindi 18 vya TV na redio vimerushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) ili kutoa elimu kwa jamii. Vipeperushi 902 vimetolewa, makala mbili zimeandikwa katika gazeti na kutoa elimu katika viwanja vya maonesho, maskulini na mikusanyiko ya kidini.

50. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ofisi kiutendaji, watumishi watatu wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu, wawili wamepata fursa ya kujifunza nchini Oman, mmoja Ujerumani, mmoja India na watumishi 30 wamepatiwa mafunzo ya ndani. Aidha, huduma za ofisi zimeendelea kutolewa kwa mujibu wa mahitaji. Ofisi ilipangiwa kukusanya Shilingi 153,898,644.00 katika vianzio vingine na tayari Shilingi 55,738,397.00 zimekusanywa, sawa na asilimia 36.

Chuo cha Utawala wa Umma

51. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Chuo cha Utawala wa Umma ina lengo la kuwajengea uwezo watumishi wa Umma. Mafunzo ya muda mfupi yametolewa kwa watumishi 1,144 kutoka Taasisi mbali mbali za Serikali. Mafunzo hayo yalihusu masuala ya itifaki, mikopo na vyama vya ushirika kwa watumishi wa Chuo cha Utawala wa Umma. Aidha, mafunzo ya taaluma za uongozi yalitolewa kwa Makatibu wa Wadi na Shehia, ujasiriamali, utafutaji nyenzo na mabadiliko ya kifikra yalitolewa kwa vijana wa Jeshi la kujenga Uchumi (JKU).

52. **Mheshimiwa Spika,** mafunzo ya maadili ya kazi kwa watumishi wapya yametolewa kwa watumishi 3,902 kutoka Wizara na Taasisi za Serikali zikiwemo Wizara ya Fedha na Mipango; Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo, na Uvuvi; Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar SUZA, Shirika la Umeme ZECO na ZURA.

53. **Mheshimiwa Spika,** wanafunzi 1,555 wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi za cheti na stashahada. Kati ya hao wanafunzi 421 ni watumishi wa Umma. Aidha, wanafunzi 1,073 walihitimu mafunzo na kutunukiwa vyeti katika Sherehe za Mahafali zilizofanyika mwezi Machi 2018. Watumishi tisa wameshiriki mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu, wawili katika kada ya teknolojia ya habari na mawasiliano na mmoja katika kada ya ukutubi. Lengo ni kuimarisha rasilimali watu ya Chuo cha Utawala wa Umma.

54. **Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Utawala wa Umma kimejiandaa kutoa shahada ya kwanza katika fani za Menejimenti ya Rasilimali Watu; Uhifadhi Kumbukumbu na Nyaraka; na Uhusiano wa Kimataifa na Diplomasia. Ili kufanikisha hatua hiyo, Serikali inaandaa utaratibu wa kuijengea uwezo IPA ili iweze kutekeleza jukumu hilo kwa ufanisi.

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma

55. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Kusimamia Maadili ya Viongozi wa Umma ina lengo la kusimamia maadili ya viongozi wa umma. Jumla ya fomu za viongozi 1,631 zilipokelewa na kusajiliwa sawa na asilimia 99 ya shabaha

iliyopangwa ya kupokea fomu za tamko la mali na madeni 1,650. Orodha ya viongozi waliowasilisha fomu imechapishwa katika Gazeti Rasmi la Serikali (Tangazo Nam. 8 la Februari 2018) kama kifungu cha 22 (3) cha Sheria Nam. 4/2015 kinavyoelekeza. Tume inaendelea na jukumu la kupokea fomu za viongozi wapya na wanaomaliza kutumikia nafasi zao.

56. **Mheshimiwa Spika,** uhakiki wa taarifa za mali na madeni za viongozi wa umma umeendelea ambapo jumla ya viongozi wa umma 73 walifanyiwa uhakiki wa taarifa zao Unguja na Pemba.

57. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2018, hakuna malalamiko yaliyopokelewa yanayohusika na tuhuma za uvunjwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi. Tume inaendelea kutoa elimu kwa umma, ili wananchi wenye malalamiko yanayohusiana na uvunjifu wa maadili wayawasilishe Tume.

58. **Mheshimiwa Spika,** elimu imetolewa kwa viongozi wa umma kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili, Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, changamoto zinazojitokeza wakati wa ujazaji wa fomu za tamko la mali na madeni pamoja na uhakiki wa taarifa. Jumla ya mikutano 37 imefanyika Unguja na Pemba, mikutano hiyo imewashirikisha viongozi wa umma kutoka Taasisi mbali mbali za Serikali, Kamati za Masheha na Skuli. Aidha, vipindi 21 vilitayarishwa na kurushwa hewani kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar kuhusu maadili ya viongozi wa umma. Jumla ya vipeperushi 4,000 vimeandaliwa, kuchapishwa na kusambazwa kwa viongozi na wananchi.

59. **Mheshimiwa Spika**, jumla ya watumishi wanne, wanawake wawili na wanaume wawili wamepatiwa mafunzo yaliyohusu Utunzaji wa Kumbukumbu, Ukatibu Muhtasi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika fani ya Programming. Watumishi 16 walipatiwa mafunzo ya siku moja juu ya ujazaji wa fomu za tamko la mali na madeni na changamoto zake. Kati ya hao wanawake saba na wanaume tisa. Mafunzo hayo yalitolewa na wataalamu kutoka Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutawala zimetolewa.

60. **Mheshimiwa Spika,** taarifa za mapato na matumizi kwa fungu G01 zinapatikana katika Viambatanisho nam. 1,3&4.

G02 – Mahakama

61. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki inatekelezwa na Mahakama ambapo matokeo yanayokusudiwa kufikiwa ni kuimarika kwa upatikanaji wa haki na uwajibikaji. Katika kufanikisha jukumu hilo Mahakama imesikiliza kesi mbali mbali za madai na jinai pamoja na rufaa za Mahakama Kuu. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2018 Mahakama imepokea na kusajili kesi 8,956 kutoka Mahakama zote Unguja na Pemba ***(angalia kiambatanisho nam.6a).***

62. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hicho, Mahakama Kuu imepokea mashauri mapya 206 ukijumuisha na mashauri 188 ya nyuma, imekuwa na jumla ya mashauri 394 ambapo mashauri sita yametolewa uamuzi. Kwa upande wa Divisheni ya Mahakama ya Kazi yamepokelewa mashauri

mapya 18 na kuifanya divisheni hiyo iwe na mashauri 36 ikijumlisha mashauri 18 yaliyosajiliwa kabla. Mahakama hiyo imetoa uamuzi kwa mashauri manne.

63. **Mheshimiwa Spika,** katika Mahakama za Mkoa, mashauri mapya 493 yamepokelewa na kufanya Mahakama hizo ziwe na jumla ya mashauri 781 ikijumlisha na mashauri mengine 288 yaliyosajiliwa kabla. Mahakama za Mkoa zimetolea uamuzi mashauri 74.

64. **Mheshimiwa Spika,** Mahakama za Wilaya zilipokea mashauri mapya 1,655 na kufikisha jumla ya mashauri 2735 baada ya kujumlishwa na mashauri 1080 yaliyosajiliwa kabla. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2018, Mahakama hizo zimetolea uamuzi mashauri 974.

65. **Mheshimiwa Spika,** Mahakama za Mwanzo zilipokea mashauri mapya 5,136 na kufikisha jumla ya mashauri 9,265 baada ya kujumlisha mashauri 4,129 yaliyosajiliwa kabla. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018, Mahakama hizo zimetolea uamuzi mashauri 4,715.

66. **Mheshimiwa Spika,** Mahakama ya Kadhi ya rufaa imepokea mashauri mapya 41 na kuifanya iwe na jumla ya mashauri 84 yanapojumuishwa na mashauri 43 yaliyosajiliwa kabla. Mashauri 15 kati ya hayo yametolewa uamuzi. Vilevile, Mahakama za Kadhi za Wilaya zimepokea mashauri mapya 1,243 na kuwa na jumla ya mashauri 2,388 baada ya kujumuishwa na mashauri 1145 yaliyosajiliwa kabla na mashauri 441 kati ya hayo yametolewa uamuzi.

67. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Mahakama ya Rufaa ya Tanzania ilikuwa na idadi ya mashauri tisa

yaliyo sajiliwa kutoka miaka ya nyuma. Kufikia Machi 2018, Mahakama hiyo imepokea mashauri 27 na kufikisha jumla ya mashauri 36 hadi kufikia Machi 2018. Hakuna shauri lilotolewa uamuzi.

68. **Mheshimiwa Spika,** Mahakama ya Watoto ilipokea mashauri mapya 134 na kufikisha jumla ya mashauri 187 yanapojumuishwa na mashauri 53 yaliyosajiliwa kabla. Katika kipindi cha Julai hadi Machi 2018, Mahakama hiyo imetoa uamuzi wa mashauri 44.

69. **Mheshimiwa Spika,** kwa uchambuzi huo, Mahakama imepokea na kusajili jumla ya mashauri 8,956 kutoka Mahakama zote kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2018 ambapo idadi ya mashauri yaliyosikilizwa na kutolewa uamuzi ni 6,274 sawa na asilimia 70 ***(viambatanisho nam. 6a, b&c vinatoa ufafanuzi).***

70. **Mheshimiwa Spika,** Mahakama tayari imeanza kuchukua hatua za ujenzi wa jengo jipya la Mahakama Kuu Tunguu. Hatua hizo ni pamoja na kufuatilia upatikanaji wa hati miliki ya kiwanja, kupata Mshauri Elekezi na kutayarisha eneo la kiwanja. Hatua iliyofikia sasa ni kwamba Mshauri Elekezi amekamilisha michoro ya jengo hilo na yupo katika hatua ya kutayarisha *"Bill of Quantities" (BOQ).*

71. **Mheshimiwa Spika,** jengo la Mahakama ya Wilaya Mwanakwerekwe limefanyiwa matengenezo makubwa na tayari limeshafunguliwa rasmi na Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein. Jengo hilo tayari limeanza kutumika. Ofisi yetu inatoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kuweza kulifanikisha hilo.

72. **Mheshimiwa Spika,** ili Mahakama iweze kufanikisha kazi zake za upatikanaji wa haki hapana budi kuwajengea uwezo watendaji wake. Ili kufanikisha azma hiyo, Waheshimiwa Majaji na Mahakimu kumi walishiriki katika Mkutano wa Majaji wa Jumuiya ya Madola, Jaji mmoja alishiriki Mkutano wa Kimataifa wa Majaji nchini India na Mhe. Jaji Mkuu alihudhuria Mkutano Nchini Namibia. Aidha, watumishi wapya 13 walipatiwa mafunzo elekezi *"Induction Course"* katika Chuo cha Utawala wa Umma Tunguu (IPA).

73. **Mheshimiwa Spika**, shughuli za kuadhimisha siku ya sheria kwa mwaka 2018, zilipambwa kwa kuweka mabanda ya maonesho katika viwanja vya Maisara kwa kuwajumuisha pamoja wadau wote wa sekta ya sheria ambao waliwapatia taaluma wananchi waliotembelea katika maonesho hayo. Lengo likiwa kuwaelimisha jinsi taasisi hizo zinavyofanya kazi.

74. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hicho, Tume ya Utumishi ya Mahakama ilifanya jumla ya vikao sita. Kati ya vikao hivyo, vinne kwa mujibu wa sheria na vikao vyengine viwili vilikuwa vya dharura. Katika vikao hivyo Tume iliteua nafasi ya Mrajis wa Mahakama Kuu na Naibu Warajis wawili. Hatua hiyo inatokana na aliyekua Mrajis kuteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Aidha, Tume hiyo ilikaa kujadili masuala ya nidhamu na maslahi ya watumishi.

75. **Mheshimiwa Spika**, shughuli mbali mbali za Uendeshaji na Utawala za Mahakama ziliendelea kufanyika kama ilivyopangwa na hivyo kuweza kupatikana ubora na ufanisi wa kazi zake.

G03 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu

76. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imetekeleza majukumu yake kupitia Programu ya Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria. Ofisi imeendelea kuimarisha Mfumo wa Sheria za Zanzibar kwa kushughulikia na kuandaa miswada sita ya sheria ambayo imewasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa kujadiliwa na hatimae kupitishwa. Miswada yote hiyo imetiwa saini na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na sasa ni sheria kamili zinazotumika.

77. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kwa mwaka 2017/2018 imeandaa Kanuni 12 zinazotokana na Sheria tofauti kwa lengo la kuzifanya Sheria hizo ziweze kutekelezeka kwa ufanisi zaidi. Vilevile Ofisi ya Mwanasheria Mkuu katika kuweka vyema kumbukumbu za kisheria imeandaa Matangazo ya kisheria 51 yanayohusu mambo mbali mbali ambayo yalihitaji kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

78. **Mheshimiwa Spika,** kuhusu shughuli za usimamizi wa Mikataba Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kazi ya kuishauri Serikali juu ya masuala mbali mbali ambayo Serikali ilihitaji kufunga nayo Mikataba. Jumla ya Mikataba 258 ilifanyiwa mapitio na kutolewa ushauri. Kati ya Mikataba hiyo, Mikataba 30 ni ya Ushauri elekezi, Mikataba 110 ni ya huduma, Mikataba 57 ya Ujenzi, Mikataba 59 ya Kodi na Mikataba miwili ya ushirikiano.

79. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya Hati za Maelewano (MoU) 56 zinazohusu Sekta ya Elimu, Afya, Ujenzi, Biashara, Uchumi, Kilimo na Uvuvi zilifanyiwa mapitio na kutolewa

ushauri na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Ofisi imesimamia jumla ya kesi 85 katika kesi hizo kesi kumi zimefikia hatua ya kutolewa uamuzi ambapo kati ya kesi hizo, nane Serikali imeshinda na kesi 75 zinaendelea kusimamiwa.

80. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Utawala na Usimamizi wa Fedha Ofisi imeendelea kutekeleza wajibu wake kwa kusimamia vyema watendaji na kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi kwa kuimarisha mazingira bora ya kazi, kuwapatia vitendea kazi na stahiki zao pamoja na kuwajengea uwezo. Katika kutekeleza hilo, Ofisi imenunua gari mbili na vespa moja ili kupunguza changamoto ya usafiri kwa watumishi hasa Wanasheria wanaokwenda na kurudi Mahakamani kila siku.

81. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imewajengea uwezo watumishi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Watumishi wawili wamesomeshwa katika ngazi ya shahada ya pili ya Sheria na mtumishi mmoja katika ngazi ya shahada ya kwanza ya Sheria. Vilevile kwa upande wa mafunzo ya muda mfupi watumishi wa sehemu ya hesabu, ununuzi na ukaguzi wa ndani wa hesabu wamepatiwa mafunzo kuhusu masuala ya kodi ya ongezeko la thamani, ushuru wa bidhaa na makato ya *"withholding tax"*. Vilevile mafunzo ya Uchambuzi wa Mikataba ya Ujenzi na Usimamizi wa Mikataba ya Mifumo *'Management of Contract for Supply and Installation of System'* yalitolewa kwa watendaji wa Idara ya Mikataba ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

82. **Mheshimiwa Spika,** watumishi wa Idara ya Usimamizi wa Kesi, walipata mafunzo ya Uendeshaji na Usimamizi wa Kesi za Madai pamoja na Uandishi wa Hati za Madai. Katika kuimarisha mazingira bora ya kazi, Ofisi imefanya

matengenezo madogo madogo ya jengo na kamera za kiusalama zimewekwa kwa dhamira ya kuimarisha ulinzi katika eneo hilo. Aidha, vitendea kazi mbali mbali vilinunuliwa ili kutekeleza vyema majukumu ya Ofisi.

83. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imepata jengo ambalo litatumika kuwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu – Pemba. Hatua za awali za matengenezo ya jengo hilo zinaendelea na zinatarajia kukamilika ndani ya mwaka huu wa fedha. Ofisi inatarajia kuanza rasmi kupeleka wanasheria katika Ofisi ya Pemba katika mwaka 2018/2019 mara baada ya kukamilika utaratibu wa ajira ambao unatarajiwa kufanywa mapema katika bajeti ijayo.

G04 – Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

84. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ina lengo la kuendesha na kusimamia kesi za jinai kiraia na kukuza mipango na uendeshaji wa Ofisi. Kati ya kesi za jinai 2,205 zilizofunguliwa katika mahakama mbali mbali za Unguja na Pemba, jumla ya kesi 1,068 zimetolewa uamuzi, sawa na asilimia 48.

85. **Mheshimiwa Spika,** katika kukuza Mipango na Uendeshaji, Ofisi imewapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi saba katika kada ya sheria ngazi ya shahada ya uzamili. Kati ya hao sita wanaume na mmoja mwanamke. Jumla ya wanasheria kumi walihudhuria mafunzo mbali mbali ya muda mfupi ambayo yameongeza ujuzi na taaluma ya kutekeleza vyema majukumu ya kazi.

G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria

86. **Mheshimiwa Spika,** Tume imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kukamilisha mapitio ya sheria tano, ambazo ni Sheria ya Kamati ya Uongozi namba 10/1986, Sheria ya Jumuiya namba 6/1995, Sheria ya Msimamizi wa Mirathi Sura ya 23/1925, Sheria ya Udhibiti wa Kodi Sura ya 98/1957 na Sheria ya Kuhifadhi Utamaduni wa Taifa namba 1/1973. Aidha, mapitio ya Sheria ya Mahakama Kuu namba 2/1985 na Sheria ya Mahakama za Chini namba 6/1985 yamefanyika kwa hatua ya kwanza na yataendelea kwa hatua ya pili katika mwaka 2018/ 2019.

87. **Mheshimiwa Spika,** vipindi 18 vya redio na 12 vya televisheni kupitia Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) vilirikodiwa na kurushwa hewani. Aidha, semina kuhusu mapitio ya Sheria ambazo zinawashirikisha wadau mbali mbali wakiwemo Mahakimu, Mawakili wa kujitegemea, Wanasheria wa Serikali, Walimu, Wanafunzi, Viongozi wa Dini, Askari Polisi, Asasi za kiraia zikiwemo Kituo cha Huduma za Sheria (ZLSC) na Wanasheria wa Chama cha Wanasheria Zanzibar (ZLS) zilifanyika kama zilivyopangwa. Aidha, jumla ya Wananchi 2,415 wa Wilaya zote za Unguja na Pemba walipata elimu na kushiriki katika kutoa maoni ya mapitio ya sheria hizo.

88. **Mheshimiwa Spika,** Tume inaendelea kujiimarisha kiutendaji kwa kuwapatia mafunzo watendaji wake walio katika kada tofauti, ambapo mtumishi mmoja anaendelea na mafunzo ya shahada ya pili katika fani ya Sheria chini ya udhamini wa Washirika wa Maendeleo. Mafunzo ya ndani kuhusiana na utafiti na uandishi wa sheria, uwekaji wa kumbukumbu, mafunzo ya utumishi wa umma

kuhusiana na majukumu na nidhamu katika kazi, mafunzo ya zimamoto na uokozi, na mafunzo ya huduma ya kwanza yamefanyika.

89. **Mheshimiwa Spika,** ushirikiano wa Kitaifa na Kimataifa umeimarika kwa kushiriki mikutano mbali mbali na kulipia ada za uanachama wa Umoja wa Tume za Kurekebisha Sheria za Afrika Mashariki na Kusini (ALRAESA) na Umoja wa Tume za Kurekebisha Sheria za nchi wanachama wa Jumuiya ya Madola (CALRAs).

G06 –Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

90. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake ya Kikatiba ya ukaguzi wa hesabu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kuimarisha uwezo wa watumishi kitaaluma katika fani mbali mbali za ukaguzi kama vile ukaguzi wa mazingira, *(Environmental Audit)* ukaguzi wa kompyuta, ukaguzi yakinifu *(Value for Money)* na ukaguzi wa aina nyengine.

91. **Mheshimiwa Spika,** mafunzo ya ukaguzi wa hesabu unaozingatia viwango vilivyowekwa kitaifa na kimataifa na mafunzo ya mabadiliko ya teknolojia katika mifumo ya uhasibu na ukaguzi na mafunzo ya mabadiliko ya Bajeti kwa wakaguzi kutoka katika mfumo wa vifungu *'Line Items'* kwenda mfumo unaozingatia matokeo (PBB) yametolewa.

92. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeendelea na majukumu yake ya ukaguzi wa hesabu ya mwaka 2016/2017 kwa kukagua Wizara zote za Serikali, Taasisi mbali mbali za Serikali

na miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na washirika wa maendeleo ambapo ukaguzi huo ulifuata sheria, kanuni, taratibu na muongozo wa ukaguzi. Aidha, Ripoti ya Ukaguzi ya mwaka 2015/2016 imekamilika.

93. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya watumishi 25 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi katika fani mbali mbali za ukaguzi yakiwemo mafunzo ya ukaguzi wa mafuta na gesi asilia, ukaguzi yakinifu, ukaguzi wa mazingira *'Environmental Audit'*, sambamba na mafunzo ya viwango vya ukaguzi vya kitaifa na kimataifa. Kwa upande wa mafunzo ya muda mrefu jumla ya watumishi 15 wanaendelea na masomo katika vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi. Aidha, Ofisi imendelea kuwapatia watumishi wake mafunzo ya sheria mbali mbali zinazohusiana na kazi za ukaguzi.

G07 – Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi

94. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uzuiaji wa vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi ina lengo la kutoa elimu kwa umma juu ya kuchukua hatua za kinga dhidi ya rushwa na kufanya uchunguzi wa vitendo vya rushwa.

95. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa elimu juu ya rushwa na athari zake inawafikia wananchi, Ofisi imeanzisha huduma ya kupiga simu bure *(toll-free 113)* ili kurahisisha utoaji wa huduma zake na kuwafikia wananchi katika maeneo yao. Hatua hii inasaidia sana katika kuiwezesha jamii kuripoti vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi kwa wakati, kwa faragha na kujiamini zaidi hasa kwenye matukio ya ghafla yanayotokea katika maeneo yao.

96. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeadhimisha siku ya kuzuia rushwa duniani ambayo ilijumuisha Taasisi zote zinazosimamia maadili na utawala bora. Katika kuadhimisha siku hii, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar imefanya makongamano mbali mbali yaliyowahusisha Vijana, Wakuu wa Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma, Waandishi wa Habari na Wananchi wa Wilaya ya Mkoani Pemba.

97. **Mheshimiwa Spika,** mikutano iliyolenga kukuza uelewa wa jamii kuhusu majukumu ya Mamlaka na umuhimu wa kuepuka vitendo vya rushwa imefanyika kwa Taasisi za Serikali Unguja na Pemba. Mikutano hiyo ilihusisha taasisi mbali mbali ikiwemo Wizara ya Ardhi, Maji, Nyumba na Nishati; Wizara ya kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto; Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kusini Pemba na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Aidha vipindi kumi vya redio na televisheni vilirushwa hewani kupitia ZBC ambavyo vilielezea madhara ya rushwa na athari zake kwa Taifa.

98. **Mheshimiwa Spika,** jumla ya tuhuma 151 za makosa mbali mbali yaliripotiwa, yakiwemo kuomba na kupokea rushwa, matumizi mabaya ya ofisi, matumizi ya mali za umma, kukwepa kulipa kodi na rushwa katika zabuni. Kati ya tuhuma hizo majalada 39 yamefikishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa hatua za kisheria na majalada matano yapo mahakamani. Mamlaka imefanya udhibiti wa mapato katika maeneo mbali mbali ya Ofisi za Serikali na kuokoa jumla ya Shilingi 169,028,120.00.

99. **Mheshimiwa Spika,** kufuatia kupitishwa na kuzinduliwa kwa Mkakati wa Kitaifa wa Kuzuia Rushwa na Uhujumu

wa Uchumi, Mamlaka imetoa elimu kwa Wizara, Idara na Taasisi za Umma za Unguja na Pemba ikiwa ni hatua ya kumuandaa kila mmoja wetu katika utekelezaji wa mkakati huo. Hatua za kuelimisha jamii kwa ujumla kuhusu mkakati huo zinaendelea.

100. **Mheshimiwa Spika,** mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu yametolewa kwa watendaji ndani na nje ya nchi ili kuwajengea uwezo utakaosaidia kufanikisha kazi za Mamlaka kama zilivyopangwa. Mafunzo haya yalihusisha fani mbali mbali za utaalamu wa kazi za Mamlaka na za taaluma nyengine.

101. **Mheshimiwa Spika,** huduma mbali mbali za kiuendeshaji na kiutumishi zimetolewa ikiwemo upatikanaji wa vitendea kazi, mawasiliano, usafiri, maji, umeme pamoja na matengenezo madogo madogo ya magari na jengo la Ofisi.

G08 – Kamisheni ya Utumishi wa Umma

102. **Mheshimwa Spika,** Kamisheni ya Utumishi wa Umma imeendelea na ziara za ukaguzi wa Taasisi za Umma. Ziara hizo zimeanza na zitaendelea katika Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na zimejumuisha Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Mabaraza ya Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri za Wilaya Unguja na Pemba. Vilevile, ziara hizo zitafanyika katika Ofisi za Tume nne za Utumishi za Zanzibar, ambazo ni Tume ya Utumishi Serikalini, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Tume ya Utumishi wa Baraza la Wawakilishi na Tume ya Utumishi wa Idara Maalum za SMZ.

103. Mheshimwa Spika, katika kushughulikia masuala ya Watumishi wa Umma, Kamisheni ya Utumishi wa Umma imepokea na kuyatolea uamuzi Malalamiko manane ya watumishi, sawa na asilimia 100 ya makadirio ya mwaka na Rufaa tatu za watumishi, sawa na asilimia 75 ya makadirio ya rufaa kwa mwaka.

104. Mheshimwa Spika, Kamisheni imepokea na kushughulikia mapendekezo ya miundo ya taasisi tano. Aidha, Kamisheni imeandaa Ripoti ya Hali ya Utumishi wa Umma na kuikabidhi kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na ameiwasilisha kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa hatua zinazohusika. Aidha, Kamisheni imekamilisha maandalizi ya Muongozo wa Usalama na Afya Kazini na imeuwasilisha kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali.

G09 – Tume ya Utumishi Serikalini

105. Mheshimwa Spika, Tume ya Utumishi Serikalini ina lengo la kusimamia uajiri na kuimarisha maadili na haki za Watumishi Serikalini. Jumla ya nafasi za ajira 2,481 zimetangazwa katika Wizara na Taasisi mbali mbali kupitia ZBC Redio na Televisheni, kufanyiwa usaili kwa nafasi hizo na kutolewa kibali cha ajira kwa Unguja na Pemba.

106. Mheshimiwa Spika, Tume imewaongezea muda wa utumishi watumishi 24, watumishi 29 wamebadilishwa kada, watumishi watatu wamepandishwa cheo. Pia Tume imeidhinisha ajira ya mkataba kwa watumishi 13, likizo bila ya malipo kwa watumishi watatu, watumishi 32 wamestaafu kazi kwa hiari na watumishi 381 wamestaafishwa kazi kwa

kufikia umri wa lazima na watumishi tisa wamestaafu kazi kwa maradhi.

107. **Mheshimiwa Spika,** watumishi 379 wamethibitishwa kazi, makosa ya kinidhamu kwa watumishi yamewasilishwa na kujadiliwa na tayari yameshatolewa maamuzi ambapo watumishi 102 kutoka wizara mbali mbali wamefukuzwa kazi baada ya kuthibitika wamefanya makosa ya kinidhamu, malalamiko 15 yamewasilishwa na tayari yameshatolewa uamuzi na watumishi 11 wameacha kazi ***(angalia viambatanisho nam. 7 a, b, &c).***

108. **Mheshimiwa Spika,** huduma za kiutawala na za kiuendeshaji zimetolewa ikiwemo ununuzi wa vifaa mbali mbali vya kuandikia na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi watatu wa Tume ya Utumishi Serikalini katika fani za takwimu, rasilimali watu na utawala.

MUELEKEO WA PROGRAMU ZA OFISI YA RAIS KATIBA, SHERIA, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

109. **Mheshimiwa Spika,** naomba sasa kuchukua nafasi hii kutoa maelezo ya muelekeo wa programu zinazosimamiwa na Ofisi yangu kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Vipaumbele vya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

110. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imejipanga kutekeleza vipaumbele vifutavyo:-

i. Kuanza ujenzi wa jengo la Mahakama Kuu Tunguu na jengo la Ofisi ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi;

ii. Kuwezesha shughuli za Serikali na utoaji wa huduma kufanyika kielektroniki;

iii. Kuendelea kutayarisha miongozo mbali mbali ya utumishi wa umma na kusimamia utekelezaji wake;

iv. Kutekeleza Programu ya Mabadiliko katika Sekta ya Sheria na Mabadiliko ya Utumishi wa Umma;

v. Kuimarisha usimamizi wa misingi ya utawala bora; na

vi. Kuongeza ufanisi katika utendaji kazi wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Ofisi ya Mufti wa Zanzibar na Mahakama ya Kadhi.

111. Mheshimiwa Spika, vipaumbele hivi vinaendana na Malengo Makuu ya Taifa (Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020 na Mpango wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Zanzibar – MKUZA III) pamoja na Malengo ya Kimataifa ya Maendeleo Endelevu na Sera za Kisekta. Pia, vipaumbele hivi vimezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa mwaka 2015-2020, Mwelekeo wa Sera za Chama cha Mapinduzi 2010-2020 na Hotuba za Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein wakati wa kampeni za uchaguzi 2010 na 2015.

Malengo Makuu ya Ofisi kwa mwaka wa fedha 2018/2019

112. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora imepanga kutekeleza malengo makuu yafuatayo:-

i. Kuimarisha upatikanaji wa haki na Utawala wa Sheria;

ii. Kuimarisha Miundo mbinu katika Sekta ya Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora;

iii. Kuweka Miundo ya Taasisi na kusimamia mipango endelevu ya upatikanaji wa rasilimali watu wenye sifa;

iv. Kuimarisha usimamizi wa masuala ya dini;

v. Kuimarisha utendaji kazi katika Utumishi wa Umma;

vi. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika shughuli na utoaji wa huduma; na

vii. Kuimarisha misingi ya utawala bora na maadili katika utendaji wa shughuli za Serikali.

113. **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais Katiba Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ina jumla ya Programu kuu 13 na Programu ndogo 24. Kati ya programu hizo, zipo programu kuu tano na programu ndogo tisa zinazosimamiwa na kutekelezwa kupitia Idara zilizo chini ya Katibu Mkuu;

na programu 8 kuu na 15 ndogo zinatekelezwa na Taasisi zinazojitegemea. Programu hizo zote zimegawika katika sehemu mbili kuu; ambazo ni utekelezaji wa majukumu ya msingi pamoja na shughuli za uendeshaji wa Ofisi. Maelezo kamili ya mwelekeo wa programu hizo ni kama ifuatavyo:-

G01 – Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma

114. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma inatekelezwa na programu ndogo mbili, Miundo na Mifumo ya Taasisi na Maendeleo ya Rasilimali Watu. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 programu hii itafanya yafuatayo:-

115. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Rasilimali Watu imepanga kufanya mapitio ya Mpango wa Rasilimali Watu wa miaka mitano 2017/2022, kuratibu na kusimamia vikao vya Wakurugenzi Uendeshaji na Utumishi wa Wizara za SMZ. Aidha, itaratibu na kusimamia vikao vya Maafisa Wadhamini wa Wizara za SMZ. Katika kuimarisha uwezo na uzoefu wa kiutendaji, ziara za kimafunzo na kuhudhuria mikutano ya kikanda na kimataifa itazingatiwa kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji wa fursa zaidi za mafunzo kwa watumishi wa umma. Vilevile, mafunzo kwa maafisa utumishi juu ya Sera na Sheria za Utumishi wa Umma yatafanyika pamoja na kuendesha mafunzo kwa watumishi wanaotarajiwa kustaafu.

116. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 357,900,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 198,900,000.00 zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi, Shilingi 159,000,000.00 zitatumika kwa matumizi mengineyo ***(angalia kiambatanisho nam. 2).***

117. Mheshimiwa Spika, programu ndogo ya Usimamizi wa Miundo, Mifumo na Maendeleo ya Watumishi imepanga kufanya Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkataba wa Utoaji Huduma kwa Mteja katika Wizara na Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kutoa elimu ya Upimaji utendaji kazi kwa Wizara, Mamlaka na Taasisi zinazojitegemea.

118. Mheshimiwa Spika, programu hii pia imepanga kuandaa Miundo ya Majukumu ya kazi kutokana na zoezi la Tathmini ya kazi na Madaraja, kuwajengea Uwezo Maofisa wa Idara ya Miundo ya Taasisi, kuadhimisha siku ya Utumishi wa Umma Duniani, kupitia, kuandaa na kutoa matoleo yanayohusu masuala mbali mbali ya Utumishi wa Umma, kuandaa na kutoa ripoti inayohusu matumizi ya fedha za kulipia mishahara ya watumishi wa umma kwa kila robo ya mwaka.

119. Mheshimiwa Spika, programu imeandaa mafunzo kwa watumishi wa umma juu masuala mbali mbali yanayohusu Sheria na Kanuni za Utumishi, kufanyia mapitio na kurekebisha viwango na taratibu za malipo ya posho mbali mbali katika Wizara na Taasisi za Serikali kulingana na miongozo iliyotolewa katika Sera ya Malipo ya Utumishi wa Umma.

120. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha programu kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 431,600,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 250,600,000.00 kwa matumizi ya mishahara na stahiki za watumishi, na Shilingi 181,000,000.00 kwa matumizi mengineyo ***(angalia kiambatanisho nam. 2).***

Programu ya Uimarishaji wa Mawasiliano ya Serikali

121. Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha dhana ya Serikali Mtandao ifanye kazi ilivyokusudiwa, Ofisi imejipangia kuanzisha dirisha la pamoja la mawasiliano ya Serikali pamoja na kusimamia uanzishwaji wa tovuti zilizo hai katika taasisi za umma. Aidha, Ofisi imepanga kutengeneza mfumo wa usimamizi wa masjala *(registry management system)* ambao unahusu taratibu zitakazorahisisha mawasiliano ya barua ndani ya utumishi wa umma, na mfumo wa kumbukumbu na maombi ya vibali vya watumishi wa umma kusafiri nje ya nchi. Vilevile, Idara ya Serikali Mtandao itaratibu maandalizi ya mfumo wa kielektroniki wa kusajili taarifa za mali na madeni ya viongozi wa umma. Kupitia hotuba hii ninazishauri Wizara na Taasisi za Serikali kuitumia ofisi yetu ya Serikali Mtandao kwa kupata miongozo juu ya matumizi ya mifumo ya kielektroniki wanayotaka kuitumia katika shughuli na huduma zao wanazotoa kwa umma. Aidha Idara imejipanga kufanya tathmini na ukaguzi wa vifaa na mifumo ya TEHAMA katika taasisi 35 za umma na kuandaa miongozo, kuelimisha na kujenga uwezo kwa watendaji, wanasiasa na wananchi juu ya dhana ya Serikali Mtandao.

122. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 665,100,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 289,000,000.00 kwa matumizi ya mishahara na stahiki nyengine za watumishi, na Shilingi 367,100,000.00 kwa matumizi mengineyo ***(angalia viambatanisho nam. 2 &5).***

Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora

123. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Usimamizi wa Utawala Bora na Haki za Binadamu imepanga kuendelea kuinua uelewa wa jamii katika masuala ya utawala bora, kufanya kongamano la kitaifa la utawala bora, kutayarisha jarida la utawala bora na kufanya tathmini juu ya jinsi ambavyo wananchi wanaelewa dhana ya utawala bora.

124. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 309,220,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 142,220,000.00 zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 167,000,000.00 zitatumika kwa matumizi mengineyo ***(angalia kiambatanisho nam. 2).***

Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini

125. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imepanga kukamilisha Muundo wa Ofisi na kuimarisha idara na vitengo vyake ili vikidhi mahitaji ya jamii na viendane na technolojia ya wakati tulionao. Aidha, kuimarisha shughuli za utoaji taaluma na

miongozo ya dini ili kushikamana na maadili ya kiislamu na kuwajengea uwezo viongozi wa kiislamu katika majukumu yao ya msingi na usuluhishi.

126. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha program hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 569,300,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 306,300,000.00 kwa matumizi ya mishahara na stahiki nyengine za watumishi na Shilingi 263,000,000.00 kwa matumizi mengineyo ***(angalia kiambatanisho nam. 2).***

Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora

127. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uongozi na Utawala imepanga kutengeneza Kituo cha Kuhifadhia kumbukumbu tuli za Ofisi, kuendelea kuwajengea uwezo wafanyakazi 15 kwa mafunzo ya muda mrefu na wafanyakazi 160 kwa mafunzo ya muda mfupi na yale ya ndani ya Ofisi *(in house training)* ili waweze kutekeleza vyema majukumu yao. Aidha, Idara imepanga kuimarisha usalama wa majengo, watumishi na wataka huduma kwa kuweka mfumo wa CCTV Camera na upimaji wa afya za wafanyakazi, kuimarisha matumizi ya miongozo mbali mbali ya kiutumishi ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji kwa lengo la kutoa huduma bora kwa umma, kuimarisha mfumo wa usimamizi wa fedha na ununuzi wa vifaa vya Ofisi na kutoa huduma za Uendeshaji wa Ofisi.

128. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha

mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 1,733,800,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 1,003,800,000.00 kwa matumizi ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 730,000,000.00 kwa matumizi mengineyo ***(angalia kiambatanisho nam. 2).***

129. Mheshimiwa Spika, kupitia Programu ya Mipango, Sera na Utafiti, Ofisi itaendelea kuratibu mipango, taarifa za utekelezaji na kufanya mapitio ya utekelezaji wa sera na sheria zinazosimamiwa na Ofisi, ikiwemo Sera ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Sera ya Msaada wa Kisheria, Sera ya Nyaraka, Sera ya Mafunzo, Sera ya Malipo na Sera ya Serikali Mtandao. Aidha, Mkakati wa Mabadiliko katika Sekta ya Sheria, Mabadiliko katika Utumishi wa Umma na ule wa Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi ni nyenzo muhimu ambazo Idara itazifanyia kazi. Misingi ya ufuatiliaji na tathmini na suala la kukusanya na kutumia takwimu sahihi ni miongoni mwa mambo ya kipaumbele. Aidha, Idara itaratibu tafiti katika Sekta za Utumishi wa Umma, Katiba, Sheria na Utawala Bora. Tafiti hizo ni pamoja na utafiti wa mahitaji ya mafunzo, tathmini ya mfumo wa kielektroniki wa rasilimali watu, utafiti kuhusu matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika shughuli za serikali na utoaji wa huduma, utafiti wa nafasi ya IPA katika kuimarisha Utumishi wa Umma na nyinginezo kama zilivyopangwa.

130. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha programu kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 390,580,000.00. Kati ya fedha hizo,

Shilingi 219,580,000.00 kwa matumizi ya mishahara na Shilingi 171,000,000.00 kwa matumizi mengineyo. vilevile naomba kuidhinishiwa Shilingi 1,050,000,000.00 kwa ajili ya shughuli za maendeleo ***(angalia kiambatanisho nam. 2).***

131. Mheshimiwa Spika, katika kuratibu shughuli za Ofisi ya Rais Katiba, Sheria Utumishi wa Umma na Utawala Bora – Pemba, programu hii imepanga kuendelea kuratibu shughuli za Ofisi, kutoa huduma za uendeshaji wa Ofisi, kusimamia watumishi wa umma kwa kuwajengea uwezo zaidi na kuondokana na tabia ya kufanya kazi kwa mazoea. Programu pia imepanga kutoa elimu dhidi ya mapambano ya udhalilishaji wa kijinsia, rushwa na uhujumu wa uchumi na kusimamia dhana ya Utawala Bora pamoja na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi watumishi wa Ofisi Kuu Pemba.

132. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 1,051,800,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 806,400,000.00 zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 245,400,000.00 zitatumika kwa matumizi mengineyo ***(angalia viambatanisho nam. 2 & 5).***

Taasisi Zinazopokea Ruzuku

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana

133. Mheshimiwa Spika, Program hii imepanga kuimarisha utoaji wa huduma za mirathi, ustawishaji wa mali za wakfu

na amana na uratibu wa shughuli za Iddi, Hijja na misaada ili zikidhi mahitaji ya wakati tulionao. Aidha, imelenga kuimarisha zaidi mawasiliano, mazingira ya kazi na ufanisi wa watendaji.

134. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha ruzuku ya Shilingi 968,700,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 548,900,000.00 kwa matumizi ya mishahara na stahiki za watumishi, Shilingi 419,800,000.00 kwa matumizi mengineyo. Aidha, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana itachangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali Shilingi 50,598,000.00 ***(angalia viambatanisho nam. 2 & 3).***

Chuo cha Utawala wa Umma

135. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Utawala wa Umma kimepanga kuandaa na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wa umma na watumishi wa sekta binafsi, kuandaa na kutoa mafunzo elekezi kwa watumishi wapya wanaoingia katika ajira kwa mara ya kwanza, kufanya tafiti katika utumishi wa umma na kutoa ushauri elekezi na kuandaa na kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi wa umma na wananchi wengine.

136. Mheshimiwa Spika, ili kukiwezesha chuo kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha ruzuku ya Shilingi 643,600,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 605,000,000.00 ni mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 38,600,000.00 kwa matumizi mengineyo ***(angalia kiambatanisho nam. 2).***

Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma

137. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Maadili ya Viongozi imepanga kupokea, kuhifadhi na kusajili taarifa za mali na madeni ya viongozi wa umma, kufanya uhakiki wa taarifa za mali na madeni kwa viongozi wa umma, kuelimisha viongozi wa umma na wananchi Unguja na Pemba kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili, kuadhimisha Siku ya Maadili Duniani, Kuwajengea uwezo watumishi kwa kuwapatia mafunzo mbali mbali, na kushiriki katika mikutano ya kimataifa, kikanda na kitaifa kuhusu maadili na uadilifu.

138. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha Tume ya Maadili kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha ruzuku ya Shilingi 737,400,000.00. Kati ya fedha hizo 212,400,000.00 ni mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 525,000,000.00 kwa matumizi mengineyo ***(angalia kiambatanisho nam. 2).***

G02 – Mahakama

139. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu ya Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki, Mahakama imepanga kuendelea na jukumu lake kuu la usikilizaji wa kesi na utoaji maamuzi kwa wakati, kuhakiksha mfumo wa kisasa wa kuendesha na kurikodi kesi unaimarika na kuendelea kujenga na kuyafanyia matengenezo majengo ya Mahakama Unguja na Pemba.

140. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 6,725,200,000.00. Kati ya fedha hizo Mahakama imepangiwa kutumia Shilingi 5,611,400,000.00 ambapo Shilingi 4,096,300,000.00 zitatumika kwa mishahara na Stahiki za watumishi na Shilingi 1,515,100,000.00 zitatumika kwa matumizi mengineyo. Shilingi 5,000,000,000.00 zimepangwa kutumika kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo na Shilingi 659,910,000.00 zinatarajiwa kukusanywa ili kuchangia mapato ya Serikali.

141. Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Kadhi imepangiwa kutumia Shilingi 1,113,800,000.00 ikiwa ni ruzuku kutoka serikalini. Kati ya fedha hizo Shilingi 878,800,000.00 zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 215,000,000.00 zitatumika kwa matumizi mengineyo ***(angalia viambatanisho nam. 2, 3 &5).***

G03 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

142. Mheshimiwa Spika, Programu ya Mageuzi ya Utoaji Huduma za Sheria itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuishauri Serikali masuala ya kisheria ikiwemo kuandaa mikataba ya kitaifa na kimataifa, kutayarisha miswada ya sheria, kusimamia mashauri ya madai kwa niaba ya Serikali na kuandaa Hati na Nyaraka za Kisheria. Aidha, inatarajia kuanza rasmi kupeleka wanasheria katika Ofisi ya Pemba mara baada ya kukamilika kwa utaratibu wa ajira.

143. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 2,027,400,000.00. Kati ya fedha hizo Shilingi 730,200,000.00 mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 1,297,200,000.00 kwa ajili ya matumizi mengineyo ***(angalia kiambatanisho nam. 2).***

G04 – Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

144. Mheshimiwa Spika, Programu ya Uendeshaji na Usimamizi wa Kesi za Jinai imepanga kuendesha na kusimamia kesi za jinai, kukuza mipango na uendeshaji wa Ofisi na kukiendeleza Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti. Aidha, Ofisi imejipanga kutoa elimu kwa umma kuhusu sheria mpya ya adhabu na sheria ya mwenendo wa jinai ili kujenga uelewa wa wananchi.

145. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 2,705,100,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 1,586,400,000.00 kwa matumizi mengineyo na Shilingi 1,098,700,000.00 kwa matumizi ya mishahara na stahiki za watumishi. Aidha, Shilingi 20,000,000.00 ikiwa ni ruzuku kutoka serikalini kwa Kituo cha Mafunzo ya Sheria ***(angalia kiambatanisho nam. 2).***

G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria

146. Mheshimiwa Spika, Programu ya Usimamizi wa Mapitio ya Sheria za Zanzibar imepanga kuzifanyia mapitio sheria tano, Sheria ya Mwenendo wa Kesi za Madai Sura 8/1917,

Sheria ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana namba 2/2007, Sheria ya Mahusiano Kazini namba 1/2005, Sheria ya Ajira namba 11/2005 na Sheria ya Watu Wenye ulemavu (Haki na Fursa Sawa) namba 9/2006. Aidha, utafiti na uchambuzi wa Matumizi ya Sheria za Zanzibar utafanyika na kuandaa ripoti, sheria zitatafsiriwa kwa lugha nyepesi na elimu kwa umma itatolewa. Tume itaimarisha utendaji wa kazi za Tume kwa kushirikiana na Taasisi zenye majukumu sawa na Tume Kikanda na Kimataifa.

147. Mheshimiwa Spika, Ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 1,045,200,000.00. Kati ya fedha hizo Shilingi 304,700,000.00 kwa matumzi ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 740,500,000.00 kwa matumizi mengineyo ***(angalia kiambatanisho nam. 2).***

G06 – Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

148. Mheshimiwa Spika, kupitia Programu ya Ukaguzi wa Fedha na Rasilimali za Umma, Ofisi itaendelea kukagua hesabu za Serikali na Taasisi zake zote kwa kutumia viwango vya ukaguzi vya kitaifa na kimataifa, sambamba na kuimarisha uwezo wa watumishi kitaaluma katika fani mbali mbali za ukaguzi.

149. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 3,022,200,000.00.

Kati ya fedha hizo Shilingi 1,472,200,000.00 zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 1,550,000,000.00 zitatumika kwa matumizi mengineyo. Aidha, Shilingi 50,954,000.00 zinatarajiwa kukusanywa ili kuchangia mapato ya serikali ***(angalia viambatanisho nam. 2 & 3).***

G07 – Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi

150. Mheshimiwa Spika, Programu ya Uzuiaji wa Vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi imepanga kuendelea na shughuli za uchunguzi wa makosa mbali mbali ya rushwa, kukamilisha Mpango Mkakati wa Mamlaka, kuendelea kutoa elimu kwa umma kwa lengo la kuelimisha jamii juu ya madhara ya rushwa na uhujumu wa uchumi na kutoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi wa Mamlaka.

151. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 1,590,800,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 876,000,000.00 kwa matumizi ya mishahara na stahiki za watumishi, Shilingi 614,800,000 kwa matumizi mengineyo. Aidha, Shilingi 100,000,000.00 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini ***(angalia kiambatanisho nam. 2).***

G08 – Kamisheni ya Utumishi wa Umma

152. Mheshimwa Spika, kupitia Programu ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma, Kamisheni ya Utumishi wa Umma

imepanga kutekeleza majukumu yake ya msingi katika kusimamia Utumishi wa Umma kwa kufanya ziara za ukaguzi na ufuatiliaji wa shughuli za Taasisi za Umma na kuzishauri taasisi hizo juu ya namna bora ya kutekeleza shughuli kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu za Utumishi wa Umma. Aidha, mapitio ya miongozo ya kuandaa Miundo ya Taasisi na Miundo ya Utumishi yatafanyika. Ofisi itachapisha na kusambaza Matoleo, itaandaa Ripoti ya Hali ya Utumishi wa Umma kwa Mwaka 2017/2018 na kuishauri Serikali juu ya njia za kuimarisha Utumishi wa Umma ili kuleta ufanisi. Vilevile, itapokea na kushughulikia rufaa na malalamiko ya watumishi, Mamlaka za Nidhamu na Mamlaka za Rufaa na kuyafanyia kazi Mapendekezo ya Miundo ya Taasisi na Miundo ya Utumishi kadiri yatakavyopokelewa. Kamisheni pia itafanya tathmini ya uwezo wa Kiutendaji ili kubaini uimara na udhaifu wake, pamoja na kuandaa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa kazi za Kamisheni ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Kamisheni.

153. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 1,033,000,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 380,200,000.00 kwa matumizi ya mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 652,800,000.00 zitatumika kwa matumizi mengineyo ***(angalia kiambatanisho nam. 2).***

G09 – Tume ya Utumishi Serikalini

154. Mheshimiwa Spika, Programu ya Usimamizi wa Watumishi Serikalini imepanga kuandaa na kusimamia

shughuli za ajira kwa kuzingatia sifa na vigezo vinavyostahiki, kuendelea kusimamia haki na nidhamu za watumishi serikalini ikiwa ni pamoja na kupokea na kusikiliza malalamiko ya watumishi, kusikiliza rufaa za watumishi wasioridhika na uamuzi uliotolewa na Mamlaka za Nidhamu zilizo chini ya usimamizi wa Tume, kuratibu uidhinishwaji wa ajira za mkataba, kuthibitisha kazi, kubadilisha kada, kutoa nyongeza za muda wa utumishi, likizo bila ya malipo, kustaafisha kisheria watumishi serikalini na kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi watumishi wa Tume ya Utumishi Serikalini.

155. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha program hii kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019, naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya Shilingi 529,200,000.00. Kati ya fedha hizo, Shilingi 189,100,000.00 zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi na Shilingi 340,100,000.00 zitatumika kwa matumizi mengineyo ***(angalia kiambatanisho nam. 2).***

SHUKURANI

156. **Mheshimiwa Spika**, baada ya kutoa maelezo hayo, kwa mara nyengine naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii mbele ya Baraza lako tukufu. Naomba niwashukuru kwa dhati wahusika na washirika mbali mbali wa maendeleo kwa ushirikiano mzuri walioutoa kwa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao umerahisisha utekelezaji wa malengo tuliojipangia. Miongoni mwao ni Jumuiya ya Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo ya Kimataifa (UNDP), Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Watoto (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu

(UNFPA), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuzuia Uhalifu na Madawa ya Kulevya (UNODC), Jumuiya ya Kiafrika ya Uongozi na Utawala wa Umma (AAPAM), Benki ya Dunia, Afrika Muslim Agency, na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB).

157. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia kutoa shukrani za dhati kwa Benki ya Maendeleo ya Kiislam (IDB), Mamlaka ya Wakfu wa Uturuki, Wizara ya Awkaaf ya Algeria, Serikali ya Saudi Arabia, Taasisi ya Red Crescent ya Uturuki, Taasisi ya World Monument Fund, Taasisi zinazosafirisha mahujaji na taasisi za misaada ya kheri Zanzibar. Aidha, tunawashukuru Save the Children, Nchi ya China, India, Korea, Japani, Indonesia, Uingereza, Marekani, Afrika ya Kusini, Oman, Uturuki na Misri.

158. **Mheshimiwa Spika**, namshukuru kwa moyo wote Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Khamis Juma Mwalim, Katibu Mkuu Ndugu Yakout Hassan Yakout, Naibu Katibu Mkuu anaeshughulikia masuala ya Utumishi wa Umma, Ndugu Seif Shaaban Mwinyi na Naibu Katibu Mkuu anaeshughulikia masuala ya Katiba, Sheria na Utawala Bora Ndugu George Joseph Kazi, kwa ushirikiano wao mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi yetu na katika kuandaa na kukamilisha hotuba hii.

159. **Mheshimiwa Spika,** napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Jaji Mkuu, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Mufti wa Zanzibar, Kadhi Mkuu, Mkurugenzi wa Mashtaka, Wenyeviti, Makamishna na

Wajumbe, na Watendaji Wakuu wa Tume zinazosimamiwa na Ofisi, Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa utendaji na ushirikiano wao wanaonipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya Uwaziri kwa ufanisi.

160. Mheshimiwa Spika, Ofisi inatoa shukrani kwa vyombo vinavyosimamia Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora vya Jamhuri ya Muungano kwa ushirikiano wao mwema. Vilevile tunatoa shukrani kwa Chama cha Wanasheria Zanzibar (ZLS), Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC), Chama cha Wanasheria Wanawake (ZAFELA), Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Zanzibar. Aidha, shukrani zetu ziwaendee Masheha na wananchi wote kwa jumla. Mwisho navishukuru sana vyomba vyetu vya habari kwa kazi nzuri walioifanya ya kutoa elimu na kutangaza matukio mbali mbali yanayohusu shughuli za Ofisi hii.

161. Mheshimiwa Spika, kwa ujumla naomba niwashukuru wote walioisaidia Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi. Shukrani zangu za dhati ziwaendee pia watumishi wote wa umma kwa kutekeleza vyema majukumu yao. Aidha, napenda kuwahakikishia washirika wetu wote kwamba, Ofisi itaendelea kuthamini kwa dhati michango yao ya hali na mali pamoja na ushirikiano wanaotupatia kila tunapowahitaji. Hatuna cha kuwalipa zaidi ya kusema ahsante, tunawathamini sana na tunashukuru kwa yote. Kwa niaba ya Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Serikali

ya Mapinduzi Zanzibar tunaomba mzipokee shukrani zetu, ahsanteni na Mungu awabariki.

HITIMISHO

162. **Mheshimiwa Spika,** kabla ya kumalizia hotuba yangu hii, naomba nikumbushe kuwa Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ina jukumu la kuhakikisha kuwa huduma kwa wananchi, upatikanaji wa haki kwa wakati, utawala bora na masuala ya dini yanasimamiwa ipasavyo. Kwa mnasaba huo, Mkakati wa Mabadiliko katika Sekta ya Sheria, Mkakati wa Mabadiliko katika Utumishi wa Umma na Mkakati wa Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi ni nyenzo muhimu zitakazotuwezesha kufikia malengo ya MKUZA, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020 pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu Duniani.

163. **Mheshimiwa Spika,** naomba wajumbe wa Baraza lako tukufu wachangie Hotuba hii, watushauri ipasavyo na hatimaye waiidhinishie Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora jumla ya **Shilingi 27,587,100,000.00** kwa matumizi ya mwaka wa fedha 2018/2019. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 15,126,000,000.00** kwa matumizi ya mishahara, **Shilingi 11,411,100,000.00** kwa matumizi mengineyo, na **Shilingi 1,050,000,000.00** kwa matumizi ya miradi ya maendeleo. Naomba pia Baraza lako likubali Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ichangie **Shilingi 761,453,000.00** kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ***(angalia kiambatanisho nam. 2&5).***

164. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

Kiambatanisho 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha, 2017/18 (katika ,000)

Fungu/Idara	Makadirio kwa mwaka 2017/2018				Fedha zilizopatikana				
	Jumla ya Matumizi ya Kawaida	Mishahara na Maposho	Matumizi Mengineyo	Jumla ya Fedha	%	Mishahara	%	Matumizi Mengineyo	%
Ofisi Kuu Pemba	1,020,820	850,820	170,000	704,157	**69%**	588,555	**69%**	115,602	**68%**
Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	370,315	249,915	120,400	229,591	**62%**	154,890	**62%**	74,701	**62%**
Idara ya Uendeshaji na Utumishi	1,588,806	978,806	610,000	1,203,197	**76%**	790,649	**81%**	412,548	**68%**
Ofisi ya Mufti	500,455	308,455	192,000	355,318	**71%**	224,818	**73%**	130,501	**68%**
Idara ya Miundo ya Taasisi	349,216	234,216	115,000	268,741	**77%**	179,691	**77%**	89,050	**77%**
Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu	273,092	180,092	93,000	208,954	**77%**	147,217	**82%**	61,737	**66%**
Idara ya E Government	608,144	283,144	325,000	418,570	**69%**	211,773	**75%**	206,797	**64%**
Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa	524,677	331,677	193,000	389,036	**74%**	258,260	**78%**	130,776	**68%**

Fungu/Idara	Makadirio kwa mwaka 2017/2018				Fedha zilizopatikana				
	Jumla ya Matumizi ya Kawaida	Mishahara na Maposho	Matumizi Mengineyo	Jumla ya Fedha	%	Mishahara	%	Matumizi Mengineyo	%
Idara ya Utawala Bora	233,807	133,807	100,000	181,059	**77%**	106,364	**79%**	74,695	**75%**
Mahakama	6,096,601	4,761,601	1,335,000	4,533,629	**74%**	3,586,596	**75%**	947,033	**71%**
Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali	1,646,109	752,509	893,600	1,159,827	**70%**	552,558	**73%**	607,269	**68%**
Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	2,273,500	1,378,500	895,000	1,605,070	**71%**	1,083,543	**79%**	521,527	**58%**
Tume ya Kurekebisha Sheria	584,400	233,200	351,200	457,083	**78%**	217,434	**93%**	239,650	**68%**
Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu	2,627,200	1,389,200	1,238,000	2,097,159	**80%**	1,090,963	**79%**	1,006,196	**81%**
Mamlaka ya kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi	1,334,700	754,000	580,700	910,627	**68%**	558,303	**74%**	352,323	**61%**
Kamisheni ya Utumishi wa Umma	940,300	390,600	549,700	604,298	**64%**	253,390	**65%**	350,908	**64%**

Fungu/Idara	Makadirio kwa mwaka 2017/2018				Fedha zilizopatikana				
	Jumla ya Matumizi ya Kawaida	Mishahara na Maposho	Matumizi Mengineyo	Jumla ya Fedha	%	Mishahara	%	Matumizi Mengineyo	%
Tume ya Utumishi Serikalini	511,800	191,000	320,800	377,568	**74%**	137,033	**72%**	240,535	**75%**
Ruzuku Chuo cha Utawala wa Umma	604,500	567,700	36,800	465,557	**77%**	441,517	**78%**	24,040	**65%**
Ruzuku Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	825,800	577,400	248,400	637,819	**77%**	426,290	**74%**	211,529	**85%**
Ruzuku Tume ya Maadili ya Viongozi	579,268	79,268	500,000	419,272	**72%**	69,272	**87%**	350,000	**70%**
Ofisi ya Hakimiliki	260,000	100,000	160,000	191,286	**74%**	74,925	**75%**	116,361	**73%**
Ruzuku DPP	55,600		55,600	32,450	**58%**			32,450	**58%**
JUMLA KUU	**23,809,110**	**14,725,910**	**9,083,200**	**17,450,269**	**73%**	**11,154,040**	**76%**	**6,296,229**	**69%**
JUMLA G01	**5,548,600**	**3,630,200**	**1,918,400**	**4,027,896**	**73%**	**2,731,489**	**75%**	**1,296,407**	**68%**
JUMLA G02 -G09	**16,014,610**	**9,850,610**	**6,164,000**	**11,745,261**	**73%**	**7,479,820**	**76%**	**4,265,441**	**69%**
JUMLA YA RUZUKU	**2,245,900**	**1,245,100**	**1,000,800**	**1,677,112**	**75%**	**942,731**	**76%**	**734,380**	**73%**

Kiambatanisho 2: Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka 2018/19 (,000)

FUNGU /IDARA	KAZI ZA KAWAIDA			KAZI ZA MAENDELEO		
	JUMLA	MISHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	SMZ	JUMLA MAENDELEO	JUMLA KUU
G02 Mahakama	5,611,400	4,096,300	1,515,100		-	5,611,400
G03 Ofisi ya M/Mkuu	2,027,400	730,200	1,297,200			2,027,400
G04 Ofisi ya M/Mashtaka	2,685,100	1,586,400	1,098,700			2,685,100
G05 Tume ya K/Sheria	1,045,200	304,700	740,500			1,045,200
G06 Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu	3,022,200	1,472,200	1,550,000			3,022,200
G07 Mamlaka ya kuzuia Rushwa	1,590,800	876,000	714,800	500,000	500,000	2,090,800
G08 Kamisheni ya Utumishi wa Umma	1,033,000	380,200	652,800			1,033,000
G09 Tume ya Utumishi Serikalini	529,200	189,100	340,100			529,200
G01 Idara ya Uendeshaji na Utumishi	1,733,800	1,003,800	730,000			1,733,800

FUNGU /IDARA	KAZI ZA KAWAIDA			KAZI ZA MAENDELEO		
	JUMLA	MISHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	SMZ	JUMLA MAENDELEO	JUMLA KUU
G01 Ofisi Kuu Pemba	1,051,800	806,400	245,400			1,051,800
G01 Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	390,580	219,580	171,000	500,000	500,000	890,580
G01 Ofisi ya Mufti	569,300	306,300	263,000			569,300
G01 Idara ya Utawala Bora	309,220	142,220	167,000			309,220
G01 Idara ya E Government	665,100	298,000	367,100	50,000	50,000	715,100
G01 Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu	357,900	198,900	159,000			357,900
G01 Idara ya Miundo ya Taasisi	431,600	250,600	181,000			431,600
G01 Ruzuku Chuo cha Utawala wa Umma	643,600	605,000	38,600			643,600
G01 Ruzuku Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	968,700	548,900	419,800			968,700
G01 Ruzuku Mahakama ya Kadhi	1,113,800	898,800	215,000			1,113,800
G01 Tume ya Maadili ya Viongozi	737,400	212,400	525,000			737,400

FUNGU /IDARA	KAZI ZA KAWAIDA			KAZI ZA MAENDELEO		
	JUMLA	MISHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	SMZ	JUMLA MAENDELEO	JUMLA KUU
G04 Ruzuku Ofisi ya M/Mashtaka	20,000		20,000			20,000
Jumla ya Ruzuku G01	**2,349,700**	**1,366,300**	**983,400**			**2,349,700**
Jumla ya Ruzuku G02-G09	**1,133,800**	**898,800**	**235,000**			**1,133,800**
Jumla ya Ruzuku	**3,483,500**	**2,265,100**	**1,218,400**			**3,483,500**
Vote G01	**5,509,300**	**3,225,800**	**2,283,500**	**1,050,000**	**1,050,000**	**6,559,300**
Jumla G01& Ruzuku G01	**5,532,000**	**2,265,100**	**3,266,900**			**5,532,000**
Vote G02 - G09	**17,544,300**	**9,635,100**	**7,909,200**		-	**17,544,300**
Jumla G1 - G9	**23,053,600**	**12,860,900**	**10,192,700**	**1,050,000**	**1,050,000**	**24,103,600**
Jumla Kuu	**26,537,100**	**15,126,000**	**11,411,100**	**1,050,000**	**1,050,000**	**27,587,100**

Kiambatanisho 3: Makusanyo ya Mapato kwa Julai/Machi 2017/2018 na Makadirio ya 2018/2019

IDARA /TAASISI	MAKADIRIO 2017/2018	MAKUSANYO HALISI	%	MAKADIRIO 2018/2019
G01 KAMISHENI YA WAKFU NA MALI YA AMANA	130,084,000	37,239,432	29	50,589,000
GO2 MAHAKAMA	500,000,000	387,083,007	77	659,910,000
G06 OFISI YA CAG	84,555,000	22,000,000	26	50,954,000
JUMLA	**714,639,000**	**446,322,439**	62	**761,453,000**

Kiambatanisho 4: Upatikanaji wa Fedha za Maendeleo kwa Kipindi cha Julai 2017 - Machi 2018

	Fedha zilizotengwa (,000)			Fedha zilizopatikana (,000)		
Jina la Mradi	**Mchango wa Serikali**	**Mchango wa Wahisani**	**Jumla**	**Mchango wa Serikali**	**Mhisani**	**Jumla Kuu**
Programu ya Mabadiliko ya Sekta ya Sheria	100,000	1,025,382	1,125,382	80,000	94,080	174,080
Mradi wa Ujenzi wa Mahakama Kuu Tunguu	900,000	0	900,000	100,000	0	100,000
JUMLA KUU	**1,000,000**	**1,025,382**	2,025,382	180,000	94,080	274,080

Kiambatanisho 5: Miradi ya Maendeleo 2018/2019

Programu	Jina la Mradi	Mchango wa Serikali
G02	Ujenzi wa Jengo la Mahakama Kuu Tunguu *	5,000,000,000
G01	Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria	500,000,000
G01	Mradi wa Serikali Mtandao	50,000,000
G01	Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi	500,000,000
	JUMLA ILIYOTENGWA WIZARANI	**1,050,000,000**
	JUMLA KUU	**6,050,000,000**

Kiambatanisho 6a:- Ufunguaji wa Kesi Mahakamani 2017/2018

	KESI ZILIZO FUNGULIWA					RUFAA			
		Madai		Jinai		Madai		Jinai	
Mahakama	**Jumla Zilizofunguliwa**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**
Mahakama ya Rufaa Tanzania	27	0	0	0	0	16	0	11	0
M/Kuu Vuga	180	43	1	14	0	98	1	25	5
M/Kuu Pemba	26	5	0	1	0	18	0	2	0
Mahakama ya Kazi	18	18	4	0	0	0	0	0	0
M/Kadhi Rufaa	35	0	0	0	0	35	13	0	0
M/ Kadhi Rufaa P	6	0	0	0	0	6	2	0	0
M/ Mkoa Vuga	287	11	2	272	39	0	0	4	0

	KESI ZILIZO FUNGULIWA					RUFAA			
		Madai		Jinai		Madai		Jinai	
Mahakama	**Jumla Zilizofungu liwa**	**Zilizofu nguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofungu liwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofu nguliwa**	**Zilizotolew a Uamuzi**	**Zilizofungu liwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**
M/Mkoa Mfenesini	55	1	0	54	9	0	0	0	0
M/ Mkoa Mwera	57	2	0	55	6	0	0	0	0
M/ Mkoa Chake	56	0	0	56	5	0	0	0	0
M/ Mkoa Wete	38	0	0	38	13	0	0	0	0
M/Wilaya Mwanakwerekwe	433	29	0	401	231	3	0	0	0
M/Wilaya Mwera	226	7	0	219	174	0	0	0	0
M/Wilaya Mkokotoni	246	1	0	245	114	0	0	0	0
M/Wilaya Mfenesini	115	0	0	115	47	0	0	0	0

	KESI ZILIZO FUNGULIWA					RUFAA			
		Madai		Jinai		Madai		Jinai	
Mahakama	**Jumla Zilizofunguliwa**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**
M/Wilaya Makunduchi	39	0	0	39	17	0	0	0	0
M/ Wilaya Mkoani	207	1	0	206	167	0	0	0	0
M/ Wilaya Chake	177	3	0	174	121	0	0	0	0
M/ Wilaya Wete	172	4	0	168	85	0	0	0	0
M/ Wilaya Konde	43	0	0	43	18	0	0	0	0
M/Watoto Vuga	95	65	27	30	10	0	0	0	0
M/Watoto Mahonda	15	6	0	9	0	0	0	0	0

	KESI ZILIZO FUNGULIWA					RUFAA			
		Madai		Jinai		Madai		Jinai	
Mahakama	**Jumla Zilizofungu liwa**	**Zilizofu nguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofungu liwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofu nguliwa**	**Zilizotolew a Uamuzi**	**Zilizofungu liwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**
M/Watoto Chake	19	0	0	19	4	0	0	0	0
M/Watoto Wete	5	0	0	5	3	0	0	0	0
Jumla	**2577**	**196**	**34**	**2163**	**1063**	**176**	**16**	**42**	**5**

Kiambatanisho 6b: Ufunguaji wa Kesi katika Mahakama za Mwanzo 2017/2018

Ufunguaji wa Kesi Mahakama za Mwanzo					
Mahakama ya Mwanzo		**Kesi za Madai**		**Kesi za Jinai**	
	Jumla	**Zilizo funguliwa**	**Zilizo amuliwa**	**Zilizo funguliwa**	**Zilizoamuli wa**
Manispaa Malindi	Jinai tu (841)	0	0	841	841
Manispaa Chakechake	Jinai tu (0)	0	0	0	0
Mwanakwerekwe	2534	76	22	2458	2431
Mwera	72	18	9	54	48
Mfenesini	482	13	5	469	461
Mkokotoni	308	9	4	299	239
Makunduchi	50	15	7	35	29

Ufunguaji wa Kesi Mahakama za Mwanzo					
Mahakama ya Mwanzo		**Kesi za Madai**		**Kesi za Jinai**	
	Jumla	**Zilizo funguliwa**	**Zilizo amuliwa**	**Zilizo funguliwa**	**Zilizoamuli wa**
Chwaka	106	7	3	99	83
Mkoani	110	22	6	88	70
Kengeja	5	1	1	4	2
Chake chake	294	17	1	227	153
Wete	186	8	0	178	168
Konde	148	8	2	140	130
JUMLA	**5136**	**194**	**60**	**4892**	**4655**

Kiambatanisho 6c: Ufunguaji wa Kesi katika Mahakama za Kadhi 2017/18

Ufunguaji wa Kesi Mahakama za Kadhi		
Mahakama za Kadhi Wilaya	**Kesi za Madai**	
	Zilizofunguliwa	**Zilizotolewa uamuzi**
Mjini	628	127
Mwera	49	22
Mfenesini	81	26
Mkokotoni	69	57
Makunduchi	23	13
Chwaka	0	0
Mkoani	65	28
Kengeja	10	5
Chakechake	154	114
Wete	105	27
Konde	59	22
JUMLA	**1243**	**441**

Kiambatanisho 7a: Malalamiko ya Watumishi Kuanzia Julai – Machi 2017/2018

S/N	Wizara/Taasisi	Idadi ya Watumishi	Aina ya Lalamiko Lililowasilishwa	Uamuzi Uliofikiwa na Tume
1	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	2	Kuomba kurudishwa kazini	Madai yamekubaliwa na wahusika wamepatiwa haki zao.
2	Wizara ya Fedha na Mipango	10	Kusimamishwa kazi kwa tuhuma za upotevu wa fedha za Serikali	Madai yao ni katika makosa ya jinai
3	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	2	Kuomba kurudishwa kazini	Madai yamekubaliwa na wahusika wamerejeshwa kazini
4	Wizara ya kazi uwezeshaji Vijana Wanawake na Watoto	1	Kusimamishwa kazi	Dai limekubaliwa na mhusika amerejeshwa kazini
	JUMLA	**15**		

Kiambatanisho 7b: Watumishi Walioajiriwa Kuanzia July, 2017 Hadi Kufikia Machi, 2018

	Wizara / Taasisi	Jumla
1	Wizara ya Afya	559
2	Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	1450
3	Wizara ya Ujenzi Mawasiliano	93
4	Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ	52
5	Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto	6
6	Wizara ya Fedha na Mipango	130
7	Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko	17
8	Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi	50
9	Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais	38

Wizara / Taasisi		Jumla
10	Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	7
11	Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali	14
12	Ofisi ya Baraza la Mapinduzi	5
13	Kamisheni ya Utalii Zanzibar	3
14	Wizara ya Ardhi Maji Nishati na Mazingira	18
15	Wizara ya Habari, Utamaduni Utalii na mambo ya kale	22
16	Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar	1
17	Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	12
18	Shirika la Huduma za Maktaba	4
JUMLA		**2481**

Kiambatanisho 7c: Shughuli Za Tume ya Utumishi Serikalini 2017/2018

Wizara/Taasisi-	Kuthibitishwa Kazini	Nyongeza ya Muda wa	Kustaafu kwa Maradhi	Kustaafu kwa Lazima	Kustaafu kwa Hiari	Kubadilishwa Kada	Kuacha Kazi	Kufukuzwa Kazi	Likizo bila ya Malipo	Uajiri wa Mkataba	Kupandishwa Cheo
Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali	196	6	3	182	16	1	3	57	3	8	
Wizara ya Fedha na Mipango	10						1				3
Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo	49	1	3	10	2			1			
Wizara ya Afya		2	1	55	2	7	4	41			
Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, U/Umma na Utawala Bora	9	2		2							
Wizara Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi	39	1		74	10		1				
Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa BLM	4	1				4					

Wizara/Taasisi-	Kuthibitishwa Kazini	Nyongeza ya Muda wa	Kustaafu kwa Maradhi	Kustaafu kwa Lazima	Kustaafu kwa Hiari	Kubadilishwa Kada	Kuacha Kazi	Kufukuzwa Kazi	Likizo bila ya Malipo	Uajiri wa Mkataba	Kupandishwa Cheo
Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira	10	2		1			1				
Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais	1	3	1			1					
Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko	3			1	1						
Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji	1		1	34	1	4		1			
Chuo cha Utawala wa Umma (IPA)				1							
Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto	2	3				2					
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja	13			3		3					

Wizara/Taasisi-	Kuthibitishwa Kazini	Nyongeza ya Muda wa	Kustaafu kwa Maradhi	Kustaafu kwa Lazima	Kustaafu kwa Hiari	Kubadilishwa Kada	Kuacha Kazi	Kufukuzwa Kazi	Likizo bila ya Malipo	Uajiri wa Mkataba	Kupandishwa Cheo
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi	1										
Tume ya Uchaguzi		2		3							
Tume ya Mipango										2	
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	4			1			1				
Kamisheni ya Utalii						1					
Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ	3			11		5					
JKU	21										
SUZA										3	
Shirika la Nyumba				3							
Shirika la Huduma za Maktaba						1					

Wizara/Taasisi-	Kuthibitishwa Kazini	Nyongeza ya Muda wa	Kustaafu kwa Maradhi	Kustaafu kwa Lazima	Kustaafu kwa Hiari	Kubadilishwa Kada	Kuacha Kazi	Kufukuzwa Kazi	Likizo bila ya Malipo	Uajiri wa Mkataba	Kupandishwa Cheo
Mamlaka ya Mji Mkongwe								1			
Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	13	1									
Baraza la Manispaa								1			
Jumla	**379**	**24**	**9**	**381**	**32**	**29**	**11**	**102**	**3**	**13**	**3**

Kiambatanisho 8a: Idadi ya Wafanyakazi ORKSUUUB Machi 2018

Idara	Unguja			Pemba			Jumla Kuu
	W/me	W/ke	Jumla	W/me	W/ke	Jumla	
Idara zilizo chini ya Katibu Mkuu							
Idara ya Uendeshaji na Utumishi	46	38	84	18	18	36	120
Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	8	7	15	4	1	5	20
Idara ya Mipango ya Rasilimali Watu	8	8	16	3	1	4	20
Idara ya Miundo ya Taasisi na Maslahi ya Watumishi	9	5	14	3	1	4	18
Idara ya Utawala Bora	2	9	11	2	3	5	16
Idara ya Serikali Mtandao	12	8	20	0	0	0	20
Ofisi ya Mufti Mkuu	10	16	26	10	5	15	41
JUMLA	**95**	**91**	**186**	**40**	**29**	**69**	**255**

Kiambatanisho 8b: Idadi ya Wafanyakazi katika Taasisi Zinazojitegemea 2018

Taasisi Zinazojitegemea	Unguja			Pemba			Jumla Kuu
	W/me	W/ke	Jumla	W/me	W/ke	Jumla	
Afisi ya Mwanasheria Mkuu	34	21	55	0	0	0	55
Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	38	14	52	20	8	28	80
Kamisheni ya Utumishi wa Umma	16	15	31	0	0	0	31
Tume ya Kurekebisha Sheria	11	11	22	0	0	0	22
Tume ya Utumishi wa Umma	6	9	15	0	0	0	15
Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma	10	11	21	0	0	0	21
Ofisi ya Mkurugenzi Mashtaka	59	30	89	10	10	20	109
Mthibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali	43	49	92	25	11	36	128
Chuo cha Utumishi wa Umma	42	22	64	0	0	0	64
Mahakama Kuu	175	120	295	76	40	116	411
Mamlaka ya Kuzuia Rushwa	34	36	70	16	3	19	89
Jumla	**468**	**338**	**806**	**147**	**72**	**219**	**1,025**
JUMLA UNGUJA/ PEMBA	**563**	**429**	**992**	**187**	**101**	**288**	**1,280**